# Nipashe

Jumanne Aprili 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581655

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



**Mpango** ataka haki itendeke ili kuondoa malalamiko

UKURASA 2



**Saa** mbili kibano Makonda Kamati Maadili ya CCM

UKURASA 3



**Samia** kusaidia upasuaji watoto vichwa vikubwa

UKURASA 7



BARCA WALALAMIKIA TEKNOLOJIA YA GOLI

UKURASA 22

# Vikwazo 370 uwekezaji na biashara vyafutwa

tbs



• **Ni** pamoja na tozo za TBS, OSHA, TMA, Zimamoto .... *Endelea Ukurasa 3*

## Askari polisi watia fora maandamano ya CHADEMA UK. 2



Baadhi ya viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa na mkoa wa Kagera wakiongozwa na askari polisi katika maandamano ya amani katika Kata ya Kashai, Hamgembe, Bilele Rwamishenye, Manispaa ya Bukoba, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Jinamizi la ajali latikisa, yaua 13 na kujeruhi sita UK. 2




**MICHEZO** CHAMA, AZIZ KI WAWINDWA AZAM UK.24 **MAONI,** UK.6

# Jinamizi la ajali latikisa, yaua 13 na kujeruhi sita

**Na Juliet Mkireri,** KILWA

JINAMIZI la ajali limezidi kutanda. Hivyo ndivyo ilivyo kutokana na mwendelezo wa ajali za barabarani zilizosababisha takriban vifo vya watu 73 ndani ya miezi miwili na wengine kujeruhiwa.

Sambamba na kuangamiza nguvu kazi ya taifa, ajali hizo pia zimesababisha uharibifu wa mali kutokana na magari yanayohusika katika ajali hizo kuteketea na kuharibika kabisa.

Jana, mathalan, watu 13 walifariki Dunia katika ajali iliyotokea kijiji cha Somanga, kata ya Somanga, tarafa ya Miteja, Kilwa mkoani Lindi baada lori aina ya HOWO kugongana uso kwa uso na basi dogo la abiria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, John Emori, alisema ajali hiyo ilitokea majira ya saa moja asubuhi huku akibainisha kuwa chanzo cha ajali hiyo ni lori kuhama eneo la lake na kwenda njia ya gari dogo hivyo kusababisha magari hayo kugongana uso kwa uso.

Alisema watu 11 walifariki dunia eneo la ajali na wawili walifia katika Kituo cha Afya cha Tingi wilayani Kilwa wakati wanapatiwa matibabu.

Alisema Jeshi la Polisi linamshikilia dereva wa lori hilo, Abdallah Hamis (37), mkazi wa Mbagala, Dar es Salaam.

Ajali hiyo imetokea huku kumbukumbu ya ajali iliyoua wanafunzi 11 jijini Arusha ikiwa bado haijafutika vichwani mwa Watanzania baada ya ajali ya Aprili 2, mwaka huu, iliyosababisha basi la wanafunzi wa Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Ghati Memorial, kusombwa na maji na kutumbukia kwenye korongo lililojaa maji katika eneo la Dampo.

Kabla ya ajali hiyo iliyogharimu maisha ya wanafunzi, kulikuwa na mfululizo wa matukio ya ajali zilizosababisha vifo vya watu kadhaa na wengine kujeruhiwa.

Machi 26, mwaka huu, waandishi wa habari wawili kutoka mkoa wa Lindi, walifariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka Dar es Salaam kurejea Lindi kupata ajali majira ya saa 7:00 usiku eneo la Nyamwage, Rufiji mkoani Pwani.

Waandishi waliofariki dunia katika ajali hiyo ni Abdallah Nanda wa Channel 10 na Josephine Kibiriti wa Sahara Media Group.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Protas Mutayoka, akitaja chanzo cha ajali hiyo kuwa ni uzembe wa dereva wa lori ambaye baada ya ajali alikimbia kwa kuwa eneo hilo la ajali halikuwa na changamoto yoyote ya miumdombinu inayoweza kusababisha tukio kama hilo.

Ajali hiyo ilitokea zikiwa siku chache katika mkoa wa Pwani iliyotokea macho 10, mwaka huu, baada baso la abiria aina ya Toyota Coaster kugongana uso kwa uso na lori katika eneo la Kiromo, wilayani Bagamoyo na kusababisha vifo vya watu tisa na wengine watatu kujeruhiwa.

**VIFO 25 ARUSHA**

Februari 24, mwaka huu, watu 25 walifariki dunia huku wengine 21 wakijeruhiwa katika ajali iliyotokea eneo la Ngaramtoni Kibaoni, Arumeru mkoani Arusha, ikihusisha lori na magari mengine madogo matatu.

Ajali hiyo ilitokea katika barabara kuu ya Arusha - Namanga baada ya magari hayo madogo kugongana na lori lenye namba za usajili KAC 943 H aina ya Mack lenye tela namba za usajili ZF 6778 mali ya kampuni ya KAY Construction ya Nairobi, Kenya.

Magari mengine yaliyohusika katika ajali hiyo ni Nissan Caravan lenye namba za usajili T 623 CQF, Mercedes Benz Saloon lenye nama za usajili T 879 DBY na Toyota Coaster yanye namba T 673 DEW, mali ya shule ya New Vision.

Watu waliofariki katika ajali hiyo walikuwa wanaume 14, wanawake 10 na mtoto mmoja. Miongoni mwa waliofariki dunia walikuwa raia saba wa kigeni.

Kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi, chanzo cha ajali hiyo kilikuwa kufeli breki ya lori, hali iliyosababisha gari hilo kuyagonga magari mengine yalikuwa mbele yake.



Mjumbe wa Bodi ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), Dk. Joyce Bazira akikabidhiwa vitendea kazi na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi (kulia), wakati wa hafla ya kumuaga Katibu Mtendaji wa zamani na kumkaribisha Katibu Mtendaji mpya, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya MCT, Jaji Robert Makaramba (wa pili kulia) na Katibu Mtendaji wa Baraza, Ernest Sungura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

DUA KULIOMBEA TAIFA

## Mpango ataka haki itendeke kuondoa malalamiko

**Paul Mabeja na Pilly Kigome,** DODOMA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, ametaka malalamiko ya watu kuwa haki haitendeki ikiwamo mauaji ya raia pamoja na kuteswa yasikaliwe kimya bali yatolewe taarifa kwenye vyombo vya sheria ili hatua zichukuliwe.

Dk. Mpango alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na wananchi pamoja na viongozi wa dini walioshiriki maombi na dua maalum ya kuliombea taifa na miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

"Pale ambapo kuna madai kuwa haki haitendeki, mauaji ya raia pamoja na kuteswa tusikae kusema tu kama hivi ambavyo tunafanya kama ushahidi upo tufikishe taarifa hizo kwenye vyombo vya sheria ili hatua zichukuliwe," alisisitiza Dk. Mpango.

Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliyotolewa hivi karibuni na kubainisha kuwapo na matumizi mabaya ya fedha za umma, Dk. Mpango alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa maagizo kwa wizara zote kuandika maelezo.

"Kweli masuala ya ufisadi yapo na kuhusu ripoti ya CAG, Rais tayari ametoa maelekezo kwa wizara zote kutoa maelezo na sisi wasaidizi wake hatutasita kuchukua hatua kwa yeyote atakayebainikia kuhusika kwenye ufisadi wa fedha za umma," alisema Dk. Mpango.

Kuhusu Muungano, aliwataka Watanzania kuwaenzi waasisi wa Muungano, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Shekhe Abeid Karume ili kuendelea kuutetea na kuudumisha.

Alisema Muungano umedumu kwa zaidi ya nusu karne na katika kipindi hicho changamoto hazikosekani, lakini zinapotojitokeza zinatatuliwa kupitia kamati za pamoja kwa mazungumzo ili kuendelea kuudumisha na kuulinda.

Makamu wa pili wa Rais Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Hemed Abdullah, alisema vijana wana deni la kuuendeleza Muunganoo ili vizazi vinavyokuja waukute ukiwa salama.

"Tunayo nafasi ya kufanya chochote ndani ya nchi hizi mbili kwani tunadumisha upendo hivyo tuusimamie na kuulinda Muungano huu ili na vizazi vinavyokuja viukute na kunufaika nao," alisema.

# Polisi watia fora maandamano CHADEMA

**Na Christina Mwakangale**

ASKARI Polisi jana walitia fora maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) baada ya kuwa mstari wa mbele ikiwa ishara ya kuimarisha ulinzi hali iliyofanya jambo hilo kufanyika kwa amani.

Katika baadhi ya picha zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii, askari hao, wakiwamo wa usalama barabarani, walionekana wakiwatangulia wanachama na wafuasi hao wakati wakiandamana.

Hali hiyo inazidi kuonyesha tofauti kubwa kwa sasa na nyakati zilizopita ambapo kulikuwa na mivutano baina ya viongozi, wanachama na wafuasi wa vyama vya upinzani upande mmoja na askari polisi upande mwingine.

Hata katika maandamano yaliyotangulia ya CHADEMA, yakiwamo yaliyofanyika Dar es Salaam, kulikuwa na hali ya utulivu mkubwa na amani huku polisi wakiwasindikiza na kulinda usalama.

**KAULI YA MBOWE**

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Mashujaa, mjini Bukoba, baada ya maandamano aliyoyaongoza kuanzia Mafumbo Centre, Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alieleza kukerwa na tabia ya baadhi ya viongozi wa serikali na watumishi wa umma, kumsifia Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye kila jambo wanaloliezea kwa wananchi huku akitaja kitendo hicho kuwa ni 'uchawa'.

Mbowe alisema kitendo hicho kinampunguzia sifa Rais Samia na kwamba miongoni mwa maneno aliyowahi kumwambia Rais alipokutana naye na kufanya mazungumzo, ni kuachana na sifa anazopewa na viongozi hao, akiwataja kuwa ni 'chawa' watakaomgharimu baadaye.

"Unakuta kila anayeongea anasema fedha hii ya ujenzi ametoa 'mama'. Niliwahi kumwambia hii tabia ya kukusifia kila jambo, eti fedha umetoa wewe, itakugharimu. hao ni chawa.

"Nchi ina hali ngumu na hali hiyo inatokana na serikali kutosikiliza maoni ya wananchi. Gharama kubwa za maisha zinatokana na tozo na kodi kubwa inayotozwa na serikali huku chawa kazi yao ni kusifia tu wakati hali ya maisha ngumu," alisema.

Mbowe alisema hatua ya chama hicho kufanya maandamano ni kupaza sauti za wananchi wasio na pa kusemea ili kufikisha ujumbe kwa serikali kufanya mabadiliko na maboresho ya maeneo kadhaa ikiwamo kushusha gharama za maisha.

"Mimi ninaendelea na maandamano. Kesho (leo) naenda Kahama, kila mmoja anaenda eneo lake. Lissu anaanza Arusha, Babati, Singida, Dodoma, Dar es Salaam tutakutana kupeana taarifa, sasa hivi ni 'bampa to bampa'. Tunafanya kwa makini kuleta mabadiliko ya nchi yetu."

"Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imeshindwa kulinda mali, rasilimali, nyingi zinapewa wageni. Kwa kipindi cha miaka 60 ujenzi wa barabara kumpa mgeni kandarasi ujenzi ni aibu, CHADEMA hatutafanya hivyo.

"Makampuni yote ya Kitanzania yaliyojenga barabara kuanzia mwaka 2014 yamefanya kandarasi za zaidi ya Sh. bilioni 633 nchi nzima. Tanzania shamba la bibi, wanapewa wageni ambao wamelipwa Sh. trilioni 11 kwa sababu zinalipwa kama fedha ya kigeni," alisema.

Mbowe alisema amebaini kampuni 10 za kigeni zimepewa kazi ya kujenga barabara na hujenga kwa viwango duni, jambo linalosababisha kuharibika ndani ya muda mfupi. Alisema kampuni hizo zinapaswa kufanya kazi kwa ubia na wazawa.

"Hebu fikiria habari ya kikokotoo kwa watumishi, wabunge wanakaa Dodoma kuzungumzia na kuibua mafao ya wake wa wastaafu wa viongozi. Kagera tupate majimbo sita tulete mabadiliko," alisema.

Mbowe alisema kitendo hicho kinatokana na bunge kuwa na idadi kubwa ya wabunge wa chama kimoja ambao hupitisha jambo lenye maslahi mapana ya nchi kwa manufaa ya wachache.

HABARI KITAIFA

# Vikwazo 370 uwekezaji vyafutwa

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kufutwa kwa tozo, ada na faini 374 zilizobainika kukwamisha shughuli za uanzishwaji wa biashara na uwekezaji ili kusaidia ongezeko la fursa za uwekezaji nchini.

Tozo hizo zinahusisha taasisi mbalimbali zikiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (OSHA), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2024/25.

Alisema pamoja na uondoshwaji wa tozo hizo, pia serikali imeunganisha mamlaka za urekebishaji ambazo majukumu yake yalionekana kuingiliana. Alitaja mfano wa majukumu hayo kuwa ni pamoja na majukumu yaliyokuwa chini ya TFDA yalihamishiwa TBS.

Pia alisema majukumu ya kutoa vibali vya kusafirisha kemikali yamehamishiwa kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, hivyo kuondoa mwingiliano uliokuwapo kati ya taasisi hiyo na TMDA pamoja na TANROADS.

Aidha, alisema serikali imefanyia marekebisho ya Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) Sura ya 415 ili kuondoa haki pekee (exclusive mandate) ya uondoshaji na usafirishaji (clearing and forwading) wa shehena kwa njia ya maji.

Alisema TASAC sasa inahusika na bidhaa nne pekee ambazo ni makinikia, wanyama hai, kemikali zinazotumika migodoni na nyara za serikali.

Prof. Mkumbo alieleza kuongezeka kwa kampuni zinazosajiliwa kutoka kampuni 7,817 mwaka 2018/19 hadi kampuni 10,656 kwa mwaka mwaka 2021/22 pamoja na kuanzishwa kwa idara inayoshughulikia biashara, viwanda na uwekezaji katika mamlaka za serikali za mitaa.

**VIPAUMBELE 2024/25**

Kuhusu vipaumbele vya Wizara hiyo kwa mwaka 2024/25, Prof. Mkumbo alisema pamoja na mambo mengine, imepanga kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Pia alisema wanatarajia kukamilisha uandaaji wa sera mpya ya uwekezaji na mkakati wake wa utekelezaji pamoja na uunganishaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje (EPZA) na kuanzisha Taasisi mpya ya kusimamia masuala ya Uwekezaji wa sekta Binafsi.

Kadhalika, alisema wizara inatarajia kuendelea kusimamia utekelezaji wa mageuzi katika uendeshaji wa mashirika ya umma, ikiwamo kuendelea kubaini mashirika ambayo majukumu yake yamepitwa na wakati au yanaingiliana na majukumu ya taasisi zingine na kuchukua hatua stahiki, pamoja na kuweka vigezo bayana vya upimaji wa utendaji wa mashirika ya umma.

# Saa mbili kibano Makonda Kamati ya Maadili

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, jana amewekwa kikaangoni kwa zaidi ya saa mbili na Kamati ya Maadili ya Chama cha Mapinduzi (CCM), jijini Dodoma.

Makonda alifika katika ofisi za Makao Makuu ya CCM, saa 3:15 asubuhi, kuitikia wito akiwa kwenye gari lake ya Land Cruiser V8 lenye rangi ya kijivu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Kanali mstaafu, Abdulrahman Kinana, ndiye aliyeongoza kikao hicho cha mahojiano.

Makonda aliandikiwa barua Aprili 16, mwaka huu ya kuitwa kwenye Kamati ya Maadili Aprili 20 na baadaye tarehe ilisogezwa mpaka Aprili 22 na alifika eneo hilo likiwa limeimarishwa ulinzi.

Nipashe ilishuhudia ulinzi wa kuingia katika ofisi hizo ukiwa umeimarishwa na kutoruhusu wanahabari kuingia kwenye viwanja vya ofisi hiyo.

Kamati hiyo ina jukumu la kusimamia nidhamu ya wanachama na viongozi wa CCM ndani ya mfumo wa vyama vingi.

Kwa mujibu wa kanuni za uongozi na maadili za CCM, mtu yeyote anayetuhumiwa mbele ya kamati hiyo kwa kosa lolote linalohusiana na maadili na nidhamu ya chama atasomewa na kujibu tuhuma mbele ya wajumbe wa kamati hiyo kwanza yeye mwenyewe, ama kwa kauli yake ama kwa maandishi, lakini hataambiwa nani aliyeleta tuhuma hizo, isipokuwa kama imekwisha julikana mapema kutokana na mijadala ya vikao, vyombo vya sheria au vyombo vya habari.

Kadhalika, uchambuzi wa tuhuma hizo utafanywa kwa kutumia njia mbalimbali pamoja na mashahidi watakaoweza kupatikana.

Uchunguzi utakapokamilika na endapo itadhihirika kwamba tuhuma hizo zina uzito, mtuhumiwa ataitwa mbele ya kikao cha kamati hiyo kama ni lazima, ili apate kuhojiwa ana kwa ana.

Chanzo cha kuaminika kilidai kuwa mahojiano hayo yalikuwa ya vuta nikuvute kwa zaidi ya saa mbili.

"Mahojiano yalikuwa makali sana kati ya anayehojiwa na anayehoji kwa sababu aliyekuwa anahojiwa naye alikuwa anahoji kulikuwa ni kivumbi," kilisema chanzo hicho.

Taarifa zinadai kuwa kauli za Makonda ndizo zilizosababisha kuitwa kwenye Kamati hiyo.

Ilielezwa kuwa wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Sokoine, Makonda akiwasilisha salamu za Mkoa wa Arusha, alidai kuna viongozi wakiwamo baadhi ya mawaziri wanalipa fedha watu kumtukana Rais Samia mitandaoni.

Kamati ya Maadili imeshawahi pia kuwahoji, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa CCM, Yusuph Makamba na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Hayati Bernard Membe, baada ya sauti zao kusambaa kwenye mitandao ya kijamii wakieleza jinsi CCM inavyopoteza mvuto, uendeshaji nchi na chama kilivyoshindwa kuwalinda makatibu hao dhidi ya mtu anayewachafua.

***Imeandikwa na Beatrice Shayo na Augusta Njoji (Dodoma)**

Nipashe
The Guardian

Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya **Nipashe Jumamosi, Nipashe Jumapili na The Guardian on Saturday** yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Subscription: 0625 174 714
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

# DCEA yakamata kilo 767 dawa za kulevya

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imesema katika operesheni ya wiki mbili iliyofanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga, imekamata kilogramu 767.2 za dawa za kulevya pamoja na kuwatia mbaroni watuhumiwa 21.

Imesema kati ya dawa hizo zilizokamatwa, heroin ni kilogramu 233.2, methamphetamine kilogramu 525.67 na skanka kilogramu 8.33.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alitoa taarifa hiyo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwendelezo wa operesheni wanazozifanya za kuwakamata watu wanaofanya biashara ya dawa za kulevya.

Lyimo alisema Aprili 4, mwaka huu, katika eneo la Mikwajuni jijini Tanga, watuhumiwa wawili walikamatwa wakiwa na dawa za kukevya aina ya heroin gramu 329.412.

Alisema Aprili 8, katika eneo la Wailes, Temeke Mtaa wa Jeshini, Dar es Salam, walikamata kilogramu 1.49 za dawa za kulevya aina ya skanka pamoja na watuhumiwa wawili kutiwa mbaroni.

Lyimo alisema Aprili 10, mwaka huu, eneo la Zinga Bagamoyo mkoani Pwani, maofisa wa DCEA walifanya operesheni na kukamata kilogramu 424.84 za dawa za kulevya aina ya methamphetamine na watuhumiwa watatu walikamatwa.

"Siku hiyo hiyo katika eneo la Kunduchi, Dar es Salaam, maofisa wa DCEA kwa kushirikiana na maofisa wa mamlaka zingine, walimkamata mtuhumiwa mmoja akiwa na dawa za kulevya aina ya heroin gramu 158.24," alisema Lyimo.

Lyimo pia alisema Aprili 16, mwaka huu, katika Kata ya Kunduchi, Dar es Salaam, zilikamatwa kilogramu 232.69 za dawa za kulevya aina ya heroin na kilogramu 100.83 za dawa za kulevya aina ya methamphetamine zilizokuwa zinaingizwa nchini kupitia Bahari ya Hindi na watuhumiwa tisa waliokamatwa.

Pia alisema Aprili 18, mwaka huu, mtu mmoja alikamatwa eneo la Bandari jijini Dar es Salaam akiwa na kilogramu 2.12 za skanka.

"Baadhi ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya wameendelea kutumia vifungashio vyenye majina ya aina mbalimbali kusafirisha vikiwamo vya kahawa na chai kwa lengo la kukwepa kutiliwa shaka wakati wa kusafirisha dawa hizo," alisema.

Alisema kati ya watuhumiwa waliokamatwa, wengi wako katika kundi la vijana na kuonya kwamba endapo kundi hilo litaendelea kujiingiza kwenye biashara na matumizi ya dawa za kulevya, litapoteza ustawi binafsi.

Pia alisema kuna hatari kwa taifa kupoteza nguvu kazi na hatimaye kuhatarisha uchumi na usalama wa nchi na kusisitiza kuwa ni wajibu wa kila mwananchi kushiriki katika vita dhidi ya dawa za kulevya.




Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi akiweka shada la maua katika kaburi la aliyekuwa mwasisi wa chama hicho na Mpigania Uhuru, Constantine Millinga Jana alipozuru katika Makaburi ya familia yaliyoko mtaa wa Mhekela Mbinga Mjini Mkoani Ruvuma jana. **PICHA: HALFANI CHUSI**

## Nchimbi atembelea makaburi ya Kapt. Komba, mwasisi wa TANU

**Na Halfani Chusi,** NYASA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema chama kitaendelea kuenzi na kuukumbuka mchango wa Marehemu Kapteni John Komba na Mwasisi wa Tanganyika African National Union (TANU), Hayati Mzee Constantine Millinga.

Komba alikuwa mwanasiasa nguli na mtunzi wa nyimbo za CCM na aliwahi kuwa Mbunge wa lililokuwa Jimbo la Mbinga Magharibi (sasa Nyasa) mkoani Ruvuma kuanzia mwaka 2005 hadi Februari, 2015.

Katibu Mkuu huyo aliyasema hayo jana alipozuru kaburi la Kapteni Komba lililoko Kata ya Lituhi wilayani Nyasa na kisha kutoa salamu za pole kwa familia yake. Nchimbi amefanya hivyo katika mwendelezo wa ziara yake kwenye mikoa sita kwa ajili ya kukijenga chama.

Akiwa kaburini hapo, alisema chama kitaendelea kuthamini na kutambua mchango wake kwa nchi na chama kwa ujumla.

"Marehemu Komba ameshiriki kuandaa taifa, vita vya Uganda, ameshiriki kutunga nyimbo za chama ambazo kwa kiasi kikubwa mpaka leo zimechangia vijana wengi kujiunga na chama hiki.

"Chama kitaendelea kuthamini mchango na kuhakikisha yale aliyoianzisha na aliyoyaota yanatimia kwa maslahi ya chama na taifa," alisema Nchimbi aliyekuwa ameambatana na viongozi wenzake wa chama akiwamo Katibu wa Itikadi Uenezi na Mafunzo, Amosi Makalla, na Katibu wa Oganaizesheni, Issa Gavu.

Akizungumza kwa niaba ya familia, mtoto wa marehemu, Dk. George Komba, aliushukuru uongozi wa chama hicho kwa kuukumbuka mchango wa baba yake huku akisisitiza kuwa kitendo hicho kimewafariji sana.

Alikumbushia kuwa baba yake alikuwa mwanajeshi na jasiri aliyepambana kukiongoza chama hicho kupata ushindi, huku akiahidi kwamba familia hiyo itaendelea kushirikiana na chama hicho kuhakikisha kinashika dola katika uchaguzi wa mwaka huu na mwakani.

"Urithi pekee ambao baba alituachia alituambia isitokee hata mtoto mmoja akahama CCM, alikuwa mzalendo, mpambanaji na mwenye ushawishi mkubwa. "Katika jitihada zake hakuna mahali hakunyaga kwa nyimbo zake kuhamasiaha watu kuipenda CCM," alisema George aliposoma wasifu wa baba yake.

Komba alifariki dunia ghafla Februari 2, 2015, kisha akazikwa nyumbani kwake Lituhi, wilayani Nyasa.

Katika hatua nyingine, Dk. Nchimbi alizuru kaburi la Hayati Mzee Millinga katika makaburi yaliyoko nyumbani kwao, Mtaa wa Mhekela, Mbinga Mjini na kuweka shada la maua kama ishara ya kuendelea kumwombea pumziko jema.

Mzee Mllinga alifariki dunia Machi 5, 2018 na alikuwa mmoja wa waasisi wa TANU, chama ambacho kilipigania uhuru na maendeleo ya Tanganyika na baadaye kuipata Tanzania.

Akizungumza na familia na wananchi wengine, Balozi Nchimbi alisema CCM itaendelea kumuenzi na kujifunza kupitia mema yote yaliyofanywa na waasisi wa vyama vya TANU na Afro Shiraz (ASP) katika kuwa sehemu ya njia ya kuendelea kisiasa, uchumi na kuimarisha umoja na mshikamano wa nchi.

## Ugonjwa usiojulikana waua Watoto wawili

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WATOTO wawili wa familia moja wamefariki dunia huku mama yao mzazi na watoto wengine wawili, akiwamo wa umri wa mwaka mmoja, wamelazwa katika Hospitali ya Mji wa Geita kutokana na ugonjwa usiojulikana uliosababisha watu hao kuhara na kutapika.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Uwanja, Enos Chelehani, alisema tukio hili lilitokea Aprili 19, mwaka huu, ambapo walianza kuumwa Aprili 18, mwaka huu, na kuwataja waliofariki dunia kuwa ni Kelvin Marco (11) na Monderic Marco (3).

Alisema aliyeanza kuumwa ni mama wa familia ambaye alikwenda kujisaidia na kupoteza fahamu ndipo mume wake aligundua na kumsaidia na baadaye watoto walipata ugonjwa huo na kupelekwa katika Zahanati ya St. Peter ambako walitibiwa na kuruhusiwa kurudi nyumbani.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, watoto hao wakiwa nyumbani walifariki dunia na mwingine naye akawa katika hali mbaya pamoja na mama ndipo wakawapeleka katika hospitali ya mji wa Geita na kwamba wakati wakiendelea na matibabu, mtoto mwingine alifariki dunia.

Alisema baada ya serikali kupata taarifa, waliita polisi ambao walikwenda nyumbani kwa familia hiyo kisha wakawapeleka kupata huduma za afya.

Mmoja wa watoto walionusurika (jina limehifadhiwa) akizungumza na mwandishi wa habari hizi, alisema usiku wake walikula wali na matunda ya tikiti maji lakini ilipoofika usiku wa manane, walianza kuumwa tumbo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Geita, Dk. Omar Sukari, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo ambalo limechukua uhai wa watoto wawili ambao miili yao imehifadhiwa katika katika Hospitali ya Mji wa Geita.

"Walifikishwa katika hospitali hii wakiwa wanaharisha na kutapika mfululizo na sisi kama idara ya afya tunafanya uchunguzi kubaini chanzo cha kuharisha na kutapika hadi kusababisha vifo na hawa wagonjwa. Tunajua mkoa wetu una tishio la watu kuhara na kutapika, hivyo tumechukua vipimo kujua ni ugonjwa gani," alisema Dk. Sukari.

Kuhusu idadi ya waliolazwa alisema ni mama wa familia hiyo na mtoto wake wa mwaka mmoja pamoja kijana mwenye umri wa miaka 16 na kwamba miili ya marehemu itazikwa kwa tahadhari ili kuepusha kusambaa kwa ugonjwa huo.

HABARI KITAIFA

# Familia yamzungumzia Gardner ikimuaga Dar

Na Restuta James

MWILI wa aliyekuwa mtangazaji wa Clouds FM, Gardner Habashi (51), unatarajiwa kuzikwa leo katika kijiji cha Kikelelwa, Tarakea, Rombo mkoani Kilimanjaro, baada ya kuagwa jana Dar es Salaam, huku familia Ikimwelezea kuwa alikuwa mtu mwenye huruma ambaye aliwasisitiza kufanya kazi kwa bidii.

Akitoa salamu za familia katika viwanja vya Leaders jana, Dk. Celine Mandara, alisema Gardner alikuwa msaada kwa ndugu na jamaa zake na mwenyeji wa wale waliokuwa wanakuja mjini kutafuta kazi au maisha.

"Kipekee kama familia tunamshukuru sana Mungu kwa kuwa na Gardner na jamii kwa ujumla imefaidika na maisha yake. Pamoja na utumishi kwa jamii, katika ngazi ya familia alikuwa na wingi wa huruma hususani kwa wanawake. Alipenda wasionewe ila wajaliwe (wathaminiwe) sana. Alisisitiza sana kufanya kazi kwa bidii bila visingizio ili ndoto zitimie," alisema Dk. Mandara.

"Pia alikuwa mwenyeji kwa ndugu waliokuja kutafuta maisha hapa mjini na aliweza kuwaunganisha watu wengi. Alishughulika na shida na mahitaji yao kama yake. Sisi kama wadogo zake, tulifaidi sana msaada wa kifedha aliokuwa anatupatia. Dunia inaweza kumtambua vinginevyo lakini sisi kama ndugu zake tunamtambua kama msaada, destiny helper (msaada wa hatima) kwetu na anayejituma sana," aliongeza.

Katika salamu zake, Rais Samia Suluhu Hassan aliandika: "Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wafanyakazi wa Clouds Media Group kwa kuondokewa na ndugu yetu, Gardner Gabriel Habash. Mchango wa Gardner kwenye ustawi wa sekta ya habari nchini ni mkubwa, na amekuwa mnasihi wa vijana wengi. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema. Amina."

Kabla ya kuagwa na umma katika viwanja vya Leaders, mwili wake ulipelekwa katika Kanisa la Kiinjili la Kulutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Mbezi Beach, ambako ilifanyika ibada maalumu iliyohudhuriwa na umati mkubwa wa watu.

Baadhi ya viongozi walioshiriki msiba huo jana ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi, ambaye alitoa salamu za wizara akimtaka mtoto wa marehemu, Karen, kutojihisi mpweke kwa kuwa baba yake amemwacha mashangazi kutokana na baba alivyoishi na watu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alipongeza mshikamano ulioonyeshwa na watu wa makundi mbalimbali na kushauri kwamba ni vyema kushirikiana zaidi pindi mtu anapougua ili aone upendo wa wanaomzunguka.

Msiba wa Gardner umehudhuriwa na wakurugenzi, wakuu wa mikoa na wilaya, viongozi mbalimbali wa dini, wakiwamo masheikh, maaskofu na wachungaji. Miongoni mwao ni Mtume Boniface Mwamposa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda.

Mwili wake ulisafirishwa jana kwa ndege Kwenda Kilimanjaro kwa ajili ya maziko ambayo yatafanyika leo.



Waombolezaji wakishusha jeneza lenye mwili wa mtangazaji wa Clouds Media Group, marehemu Garner G Habash, kwaajili ya kuagwa katika viwanja vya Klabu ya Leaders, jijini Dar as Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kamati yashauri uwekezaji katika masoko ya hisa

**Na Vitus Audax,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imewashauri Watanzania kuongeza uwekezaji katika masoko ya hisa na taasisi binafsi zenye tija na manufaa kwa taifa.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Dk. Alice Kaijage, alisema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2023/24 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2024/25

Alisema serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake ili kuondoa hali ya baadhi ya miradi kutokupelekewa fedha kabisa za bajeti.

Pia alisema kamati inaitaka serikali kuongeza mitaji kwenye taasisi na mashirika ya umma, ili kuleta tija na kuongeza faida na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, kwa kutoa huduma kwa wafanyabiashara na wawekezaji kwenye eneo maalum katika kila mkoa.

Vilevile, alisema ili kuondoa migogoro mbalimbali na wawekezaji, serikali itenge hifadhi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji mahsusi.

"Dira ya Mpango wa Maendeleo 2050 iendane na maendeleo ya nchi na watu sambamba na kufanya mabadiliko ya mifumo ya kiutawala hususani mifumo ya serikali za mitaa na kuhimiza matumizi ya mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa miradi ya maendeleo (NPMIS ) kwa watekelezaji wa miradi ya maendelelo," alisema.

Dk. Kaijage pia alisema kamati ilifanya uchumbuzi wa matumizi ya bajeti pamoja na upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2023/24 na kubaini kuwa hadi kufikia Februari 2024, hakuna taasisi yoyote chini ya ofisi hiyo iliyopata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa asilimia 66.6.

Alisema kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, iliidhinishiwa Sh. bilioni 126.194 kwa mwaka wa fedha 2023/24 lakini hadi kufikia Februari, mwaka huu, ofisi ilipokea Sh. bilioni 57.663 pekee sawa na asilimia 46 ya bajeti iliyoidhinishiwa na bunge.

Kamati hiyo iliishauri serikali kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa na bunge kwa ofisi hiyo zinapatikana kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/24.

# Bilioni 429/- zaleta mageuzi bandari Tanga

Na Joseph Mwendapole

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imetekeleza miradi miwili mikubwa ya kimkakati kwa ajili ya kufanya maboresho makubwa kwenye bandari ya Tanga yenye thamani ya Sh. bilioni 429.1.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mrisha, wakati wa ziara ya wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari kwenye bandari hiyo.

Alisema katika mradi wa kwanza, TPA iliingia mkataba na kampuni ya China Habour Engineering Company (CHEC) ambao ulianza mwaka 2019 na kukamilika Juni, 2022 kwa thamani ya Sh. bilioni 172.3.

Mrisha alisema Oktoba 2019, TPA iliingia mkataba na kampuni za NIRAS A/S (AS A LEAD Firm) ya Denmark kwa ushirikiano na M/S Maritime & Transport Business Solution, M/S ILF Consulting Engineers na M/S Anova Consult Company Limited ya Tanzania kwa kufanya upembuzi yakinifu na kusimamia mikataba ya ujenzi wa gati pamoja na kuongeza kina katika bandari ya Tanga.

Alisema mradi huo ulihusisha upanuzi wa eneo la kuingia na kutoka bandarini lenye upana wa mita 73, uongezaji wa kina cha maji kutoka mita tatu hadi mita 13, upanuzi wa eneo la kugeuzia meli kuwa na kipenyo cha mita 800 na ununuzi wa mitambo 16 ya kuhudumia shehena.

Mradi huo wa awamu ya kwanza, alisema ulishakamilika kwa asilimia 100 na meli kubwa zimeanza kuingia na kufunga katika eneo la maegesho na mitambo inafanya kazi ya kupakia na kupakua shehena kwa ufanisi.

Katika mradi mwingine, alisema TPA iliingia mkataba na China Habour Engineering Company (CHEC) mwaka 2020 kwa ajili ya kuboresha Bandari ya Tanga.

Alisema mradi huo ulitekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za Serikali kupitia TPA chini ya Wizara ya Uchukuzi na uligharimu shilingi bilioni 256.8 ikiwa ni gharama za ujenzi kwa Mkandarasi.

Alisema kwa ujumla mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 ya utekelezaji wake na kwa sasa wako katika kipindi cha matazamio ambacho kitaisha mwezi Aprili 2024.

Mrisha alisema mradi huo una Gati lenye urefu wa mita 450, kina cha mita 13 na yadi ya makasha ya mita za mraba 7,230.

Alisema gati hilo lina uwezo wa kuhudumia meli mbili za makasha zenye urefu wa mita 220 na kubeba tani mpaka 60,000 kwa wakati mmoja.

Kuhusu ajira kwa wazawa, Mrisha alisema Mhandisi Mshauri aliajiri wahandisi wazawa wanne na kwa kada nyingine aliajiri wafanyakazi watatu wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Mrisha alisema kuhusu mkandarasi mjenzi, wafanyakazi wazawa wa kada mbalimbali walioajiriwa walikuwa kati ya 151 mpaka 581 kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi.

Alisema lengo la mradi huo ni kuimarisha na kuboresha magati mawili yenye urefu wa mita 450, kuongeza mita 50 upande wa Mashariki na mita 92 upande wa Magharibi kuelekea Baharini, ikiwa ni pamoja na kuongeza kina cha maji kutoka mita tatu hadi mita 13.

"Kabla ya kujengwa gati hili, Bandari ya Tanga ilikuwa ina uwezo wa kuhudumia tani 750,000 za shehena kwa mwaka. Lakini baada ya upanuzi, Bandari imekuwa na uwezo wa kuhudumia shehena mpaka tani 3,000,000 kwa mwaka na Makasha yameongezeka kutoka 12,000 hadi 50,000 kwa mwaka," alisema.

Alisema wanatarajia kuongezeka kwa shehena ya mizigo kutokana na kuongezeka kwa ufanisi kwa kupunguza muda wa kuhudumia meli kutoka siku tano hadi siku mbili na kupungua kwa gharama za uendeshaji kutokana na uwezo wa Bandari ya Tanga kuhudumia meli gatini.

Mrisha alitaja sababu nyingine kuwa ni kuongezeka kwa wateja walioonesha nia ya kuitumia Bandari ya Tanga kwa Makampuni mbalimbali na kuongezeka kwa ufanisi na tija katika kuhudumia shehena ya mizigo mbalimbali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rais kugharamia upasuaji watoto 100 ni faraja

**TATIZO** la watoto kuzaliwa na tatizo la vichwa vikubwa na mgongo wazi, linawakosesha raha wazazi wengi kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa kugharamia matibabu ya watoto wao.

Wazazi wasiokuwa na uwezo hupoteza watoto wao kwa kukosa fedha za kuwagharamia kutokana na gharama zake kuwa kubwa.

Kwa wanaotembelea hospitali kubwa kama ya Muhimbili, unaweza kushuhudia kinamama wengi wakiwa wamepakata watoto wenye matatizo hayo huku wakiwa na nyuso za kukata tamaa.

Baadhi yao huokoa watoto wao kwa kuomba msaada kutoka kwa wasamaria wema au taasisi zinazotoa msaada wa matibabu hayo.

Kauli ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwamba Rais Samia Suluhu Hassan, atagharimia matibabu ya upasuaji kwa watoto 100 wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, imeleta faraja kubwa kwa wazazi ambao walishakata tamaa ya watoto wao kupona.

Matibabu hayo kwa mujibu wa Waziri wa Afya yatakayofanyika katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI).

Waziri Ummy alitembelea Taasisi ya Mifupa (MOI) kuwajulia hali watoto 25 waliofanyiwa upasuaji chini ya ufadhili wa MO Dewji Foundation.

Kutokana na tatizo hilo la watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, Rais Samia ameguswa na ameamua kugharamia matibabu ya watoto hao ili kuepusha madhara na ulemavu unaoweza kusababishwa na kuchelewa kufanyiwa upasuaji.

Waziri Ummy alieleza kuwa amemsikia mwenyekiti wa chama cha wazazi na walezi wenye watoto wa tatizo hilo la kichwa kikubwa na mgongo wazi kwamba wana watoto kama 200 wanaopaswa kufanyiwa upasuaji, lakini wazazi hawana uwezo.

Akasema kuwa Rais Samia amemuelekeza, alete pesa kwa ajili ya watoto 100 ambao watafanyiwa upasuaji wa kichwa kikubwa na mgongo wazi bure.

Pia, akamuagiza Mkurugenzi wa Taasisi ya MOI kuwasiliana na chama hicho kuwabaini watoto wenye tatizo hilo ndani ya wiki moja na kuahidi kuwa wizara itaketa hizo fedha.

Pamoja na jitihada za Rais Samia kusaidia watoto hao, ni vizuri pia wadau wengine wakajitokeza kusaidia juhudi hizo za Rais ili kuendelea kuokoa watoto wengi zaidi wenye tatizo hilo.

Kuna taasisi nyingi ambazo zinaweza kujitolea kwa kile wanachokipata kurudisha fadhila kwa jamii hasa kwenye matibabu kutokana na baadhi ya Watanzania kutokuwa na uwezo huo.

Kwa wazazi wenye watoto wenye tatizo hilo, wanapaswa kuwapeleka hospitali na kuachana na dhana kuwa wamelogwa na kuishia kwenda kwa waganga wa jadi ambao huwapa maelezo ya uongo na mwishowe kupoteza watoto wao.

Tatizo la vichwa vikubwa linaweza kuzuilika kwa kuhakikisha kinamama wanapokuwa wajawazito wanakula vyakula vyenye madini ya Frolic Acid na kuzingatia umuhimu wa kwenda kliniki.

Chama cha Wazazi na Walezi wa Watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi Tanzania (ASBATH), kimebainisha kuwa na orodha ya watoto 200 wanaohitaji matibabu, lakini kutokana na ukosefu wa fedha wameshindwa kupata matibabu hayo.

Idadi hiyo ni kubwa, lakini inaweza kuondolewa kwenye tatizo hilo kama Watanzania kwa umoja wao watajitoa kuwasaidia.

Kama watu wanaweza kuchangia mamilioni kwenye sherehe mbalimbali, kwanini kwenye matibabu ishindikane.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Walimu wapya wafike shule za pembezoni

Sabato Kasika

**SERIKALI** imetangaza ajira mpya za watumishi 46,000, huku katika idadi hiyo, kibali cha ajira ya walimu kikiwa ni 12,000, ambao inaelezwa kuwa wanatarajiwa kupangiwa vituo vya kazi kabla ya Juni mwaka huu.

Taarifa ya ajira hizo, inatolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora George Simbachawene, hivi karibuni bungeni jijini Dodoma.

Hatua hiyo ya kutangaza ajira hizo 46,000, inatokana na ridhaa ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa kibali cha kuajiri idadi hiyo ya watumishi, wakiwamo walimu 12,000.

Kwa sasa Tanzania ina uhaba wa walimu 271, 028 wa kuanzia elimu ya awali hadi sekondari, lakini kibali cha ajira kilichotoka ni cha walimu 12,000 maana yake ni kwamba bado wanahitajika wengine zaidi.

Iwapo wataajiriwa hao 12,000, bado kutakuwa na pengo la walimu 259,028 ili kutumia idadi 271, 028 wanaohitajika. Hivyo, ninadhani juhudi zaidi zinahitajika kukabiliana na tatizo hilo.

Idadi hiyo ya uhaba huo wa walimu, iliwahi kutajwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa Februari mwaka huu.

Waziri huyo alikuwa akizindua kituo cha ufundishaji mbadala kilichopo katika shule ya sekondari Dodoma, na kufafanua kuwa, ingewa serikali imehamisha baadhi ya walimu katika shule ambazo wapo wengi na kuwapeleka kwenye upungufu, bado kuna uhaba mkubwa wa walimu.

Ni wazi kwamba bado idadi kubwa ya walimu inatakiwa kuajiriwa, lakini ingekuwa ni vyema kama serikali itaendelea na utaratibu wake wa (msawazo) kupunguza wa walimu kutoka shule ambazo zina walimu wengi na kuwapeleka katika shule zenye upungufu zaidi.

Serikali imekuwa ikitoa ajira ili kukabiliana na upungufu wa walimu shuleni, unaotokana na walimu kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa, kufariki na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa.

Lakini bahati mbaya kwamba bado uhaba mkubwa wa walim,u hasa kwenye shule za pembezoni ambazo wakati mwingine shule moja yenye wanafunzi 800 inaweza kuwa na walimu wanne hadi nane au 10 tu.

Wakati maeneo ya vijiji hali ikiwa hivyo, inawezekana mijini kukiwa na walimu 80,000 katika shule moja, hali ambayo iliifanya serikali kuanzisha msawazo ili kuwe na uwiano.

Uwiano huo ni kati ya idadi walimu wa shule za mijini na wa vijijini ili wanafunzi wote wapate vipindi sawa vya masomo, badala ya wengine kunufaiaka na baadhi kubaki nyuma.

Kwa kuwa kasi ya kuajiri walimu inaonekana kuwa ndogo, ninadhani ipo haja kuendelea msawazo kwa kupunguza idadi ya walimu ambao waliorundikana katika shule za mijini na kuwapeleka vijijini.

Huko ndiko kwenye uhaba mkubwa unaosababisha wanafunzi wasisome masomo yote au mwalimu kurundikiwa vipindi vingi vya kufundisha na kujikuta akikosa muda wa kupumzika.

Njia hiyo ya kupunguza (msawazo) walimu katika shule mijini ikiendelea kutumika, inaweza kusaidia angalau kukabiliana na tatizo la uhaba wa walimu katika shule za vijijini huku serikali ikiendelea kujipanga kuajiri.

Ikumbukwe kwamba, hakuna elimu bila walimu, hivyo njia mbalimbali za kuwezesha kuwa na walimu wa kutosha ni za muhimu ili kukabiliana na tatizo hilo, kuanzia msawazo hadi ajira mpya.

Ndani ya changamoto hiyo, wapo baadhi ya wanafunzi wanaotembea umbali mrefu kufuata elimu, lakini wanajikuta wakikosa baadhi ya vipindi kutokana na uhaba wa walimu.

Hivyo, wanafunzi wanajikuta katika mazingira magumu, kutembea umbali mrefu na kisha kukutana na tatizo hilo la kutofundishwa masomo yote kwa sababu shule yao haina walimu wa kutosha.

HABARI KITAIFA

# Wanawake wanaomiliki ardhi waongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kupitia Mradi wa Kuboresha Usalama wa Miliki za Ardhi (LTIP), idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi nchini imeongezeka kutoka asilimia 25 hadi 41.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Rose Tweve.

Mbunge huyo alihoji serikali imefikia wapi kuweka utaratibu rahisi wa urasimishaji na umilikishaji ardhi hususani kwa wanawake.

Akijibu swali hilo, Pinda alisema serikali inatekeleza mradi huo kwa mkopo wa fedha kutoka Benki ya Dunia (WB) ambao unafanyika katika mamlaka za upangaji 58 nchini.

Kupitia mradi huo, alisema haki za wanawake zimezingatiwa ipasavyo katika utoaji wa elimu na uhamasishaji umiliki wa ardhi kwa wanawake na umiliki wa pamoja baina ya mume na mke.

"Kupitia utaratibu huo, vikosi kazi vimeundwa kwa ajili ya kushughulikia uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa makundi maalum ya wanawake, wazee na wenye ulemavu katika suala la urasimishaji makazi pamoja na umiliki wa pamoja wa ardhi," alisema.

Aidha, alisema elimu inatolewa kupitia vyama vya hiari vya kijamii, mashirika yasiyo ya kiserikali, CSO's na NGO's na mikutano ya elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa mradi imefanyika katika ngazi za mitaa, kata na wilaya.

"Wananchi 3,249 wamehudhuria mikutano hiyo wakiwamo wanaume 1,518 na wanawake 1,731. Mradi pia umewezesha kuongezeka kwa idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi nchini kutoka asilimia 25 hadi asilimia 41," alisema.

Vilevile, alisema idadi ya hatimiliki za pamoja kati ya wanandoa zimeongezeka na kufikia asilimia 10 ya hati zinazotolewa.

**"Kupitia utaratibu huo, vikosi kazi vimeundwa kwa ajili ya kushughulikia uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa makundi maalum ya wanawake, wazee na wenye ulemavu katika suala la urasimishaji makazi pamoja na umiliki wa pamoja wa ardhi," alisema.**




Mchambuzi wa sera kutoka Taasisi ya Zaina Foundation, Mwanasheria William Kahale akitoa elimu kwa waandishi wa habari na wanawake wanaofanya kazi kwenye asasi za kiraia kuhusu umuhimu wa kuwepo mtandao na njia bora kuutumia ili kutopata madhara mbalimbali ya mitandao, wakati wa semina ya siku moja iliyoandaliwa na taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Rais Samia kusaidia watoto 100 wenye vichwa vikubwa upasuaji

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS Samia Suluhu Hassan, atagharamia matibabu ya upasuaji kwa watoto 100 wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi yatakayofanyika katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI).

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema hayo alipotembelea Taasisi ya Mifupa (MOI) kuwajulia hali watoto 25 waliofanyiwa upasuaji chini ya ufadhili wa MO Dewji Foundation.

Alisema Rais Samia ameguswa na tatizo hilo na ameamua kugharamia matibabu ya watoto 100 zaidi ili kuepusha madhara na ulemavu unaoweza kusababishwa na kuchelewa kufanyiwa upasuaji.

"Nimemsikia mwenyekiti wa chama cha wazazi na walezi wenye watoto wa tatizo hili la kichwa kikubwa na mgongo wazi kwamba wana watoto kama 200 wanaopaswa kufanyiwa upasuaji, lakini wazazi hawana uwezo," alisema.



"Rais Samia amenielekeza, nilete pesa kwa ajili ya watoto 100 ambao watafanyiwa upasuaji wa kichwa kikubwa na mgongo wazi bure, Prof. Makubi wasiliana na chama chao kuwabaini watoto hawa na ndani ya wiki moja wizara italeta hizo fedha," alisema Waziri Ummy.

Aidha, aliipongea taasisi ya MOI kwa kutoa matibabu ya watoto hao na MO Dewji Foundation kwa ufadhili wa matibabu ya watoto 50, huku akiwataka wadau kuendelea kujitokeza kusaidia wengine.

"Natoa wito kwa wazazi wenzangu kwa wale wenye watoto wenye changamoto hii ya vichwa vikubwa na mgongo wazi wasiwafiche watoto hao, wahakikishe wanapeleka kliniki ili wapate ushauri wa kitaalam," alisema.

Daktari bingwa mbobezi wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu MOI, Dk. Hamisi Shabani, alisema tatizo la vichwa vikubwa linaweza kuzuilika kwa kuhakikisha wanaume wanawalisha wake zao vyakula vyenye madini ya Frolic Acid na kuwawahisha kliniki wale wenye tatizo hilo.

Mkurugenzi wa MO Dewji Foundation, Imran Sherali, alishukuru serikali na taasisi ya MOI kwa kufanikisha matibabu hayo na kuongeza kuwa taasisi hiyo iko tayari uendelea kutoa msaada kwa watoto wengine.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wazazi na Walezi wa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi Tanzania (ASBATH), alisema kwa sasa chama hicho kina orodha ya watoto 200 wanaohitaji matibabu lakini kutokana na ukosefu wa fedha wameshindwa kupata matibabu hayo.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Raia wa Liberia ahukumiwa miaka 20 jela kusafirisha dawa za kulevya

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Rufani imebariki kifungo cha miaka 20 jela na faini ya zaidi ya milioni 200 aliyoamriwa kulipa raia wa Liberia, Edwin Swen, kwa kusafirisha kete 97 zenye uzito wa gramu 1509.35 za dawa ya kulevya aina ya heroine katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Uamuzi huo ulitolewa na jopo la majaji watatu; Jaji Winfrida Korosso, Jaji Sam Rumanyika na Jaji Leira Mgonya, baada ya kutupilia mbali rufani ambayo mrufani Swen alikata kupinga hukumu ya Mahakama Kuu, iliyosikiliza kesi ya uhujumu uchumi.

Wakati wa kusikilizwa kwa rufani hiyo, wakili wa mrufani alipinga kupokewa kwa dawa hizo, akidai kuwa hazikujadiliwa katika shauri la muhamisho (comital proceedings) kama inavyotakiwa kisheria.

Baada ya kupitia kumbukumbu za rufani hiyo, majaji hao walibaini kuwa mrufani alifahamishwa wakati wa shauri hilo kuwa vielelezo hivyo halisi vitatolewa mahakamani katika kesi hiyo.

"Hivyo, mrufani alifahamishwa ipasavyo na akapewa fursa ya kujua na kuelewa mapema kiini cha kesi hiyo ili kumwezesha kujitetea. Kwa hiyo, tunakubaliana na upande wa mashtaka kwamba lalamiko hili halina msingi," walisema.

Mrufani huyo pia alilalamikia usahihi wa hukumu hiyo kwa kuwa wakati akitoa hukumu dhidi yake jaji aliyesikiliza kesi hiyo alishindwa kuzingatia miaka tisa na miezi mitano aliyokaa rumande kinyume na kifungu cha 172 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Baada ya kutafakari hoja zilizowasilishwa, majaji hao walibainisha kuwa mahakama hiyo iliendelea kumtia hatiani mrufani hadi kifungo cha miaka 20 jela, kifungo cha chini zaidi kwa kupatikana na hatia na suala la malalamiko yake lilizingatiwa.

Kulikuwa na malalamiko mengine kuhusu mlolongo wa uhifadhi wa dawa za kulevya ambazo zilikamatwa kutoka kwa mrufani kwamba zilichakachuliwa kutoka uwanja wa ndege hadi Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kabla ya kuwasilishwa mahakamani kama kielelezo wakati wa kesi.

Baada ya uchunguzi wa kina wa ushahidi huo, majaji hao walijiridhisha kuwa ushahidi unaonyesha kuwa wakiwa chini ya uangalizi katika uwanja wa ndege, akituhumiwa kusafirisha dawa za kulevya, mrufani alijisaidia haja kubwa kete 97 ambazo zilikubaliwa kama vielelezo.

"Ushahidi unaeleza wazi ukweli huu kwamba vidonge vilivyotolewa kwa njia ya haja kubwa vilivyokamatwa kwa tarehe na muda uliotajwa baadaye vilioshwa, kuwekwa kwenye mifuko nyeusi na kuhifadhiwa kwenye droo ya ofisi na (maofisa wa polisi) ambao walikuwa walinzi pekee wakati wa zamu zao za kazi," walisema.

Majaji hao walisema kwa kuchukua ushahidi huo kwa ujumla hatua kwa hatua, walijiridhisha kuwa ushahidi wa mdomo wa mashahidi wa upande wa mashtaka ulithibitisha kuwa vidonge hivyo viliwekwa chini ya ulinzi kwenye droo za Ofisi za Kitengo cha Kuthibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (ADU) katika uwanja wa ndege.

Walibainisha kuwa dawa hizo wakati wote zilikuwa chini ya ulinzi wa maafisa wa polisi kwamba hakuna nafasi au hatari ya kuathiriwa kabla ya kukabidhiwa kwa kiongozi mwandamizi wa polisi.

"Matokeo yetu yanaimarishwa zaidi na ukweli kwamba fomu za uchunguzi zilizotiwa saini na mashahidi, mrufani (na maafisa wawili wa polisi) zinaonyesha wazi idadi ya vidonge vilivyochukuliwa kwa kila tukio," majaji walisema.

Pia, walitambua ukweli kwamba uaminifu wa mashahidi ulithibitishwa na jaji wakati wa kusikiliza kesi, na hawakuona chochote cha kutowaamini. "Kinachotuongoza ni ufahamu wetu kwamba kila shahidi ana haki ya kuthibitishwa na kuaminiwa," walisema.

Wakili wa mrufani pia alipinga hukumu ya mahakama kwa kuwa haikuwa na sababu nzuri na ushahidi wa upande wa mashtaka ulikuwa dhaifu.




Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge (wa pili kulia), akipokea msaada wa kibinadamu wenye thamani ya takribani Sh. milioni 250 kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Vyombo vya Habari wa kampuni ya Vodacom Tanzania, Annette Kanora, mjini Kibiti mwishoni mwa wiki, uliotolewa na Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation kwa ajili ya wahanga wa mafuriko ya Rufiji na Kibiti. Wengine kutoka kushoto ni Meneja wa Taasisi hiyo, Sandra Oswald (kushoto) na Meneja Mauzo wa eneo hilo, Suleiman Amri (wa pili kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasimamizi wa uchaguzi kuongezewa viwango vya posho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imefanya maboresho kwa kuongeza viwango vya posho za kujikimu wasimamizi wa uchaguzi kupitia waraka wa utumishi wa umma namba moja uliotolewa Mei 24, 2022.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Angelina Malembeka.

Mbunge huyo alihoji Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu mpango wa kuongeza posho kwa askari na maofisa wasimamizi wa uchaguzi.

Katambi alijibu kuwa wakati wa uchaguzi, wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa ngazi ya jimbo na kata hulipwa posho za kujikimu wanapokuwa wanatekeleza majukumu ya uchaguzi kwa kuzingatia waraka huo.

Aidha, alisema kwa upande wa watendaji na walinzi wa vituo vya kupigia kura, utaratibu wa uboreshaji wa viwango vyao vya posho utazingatiwa wakati wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na bajeti ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Katika maswali yake ya nyongeza, Mbunge huyo alisema kwa kuwa uboreshaji wa daftari utakwenda sambamba na uboreshaji posho kwa mwaka 2025, na kuhoji serikali haioni haja ya kuanza kulipa mwaka huu katika uchaguzi wa serikali za mitaa ili kuleta motisha kwenye uchaguzi.

"Zanzibar maofisa husimamia chaguzi mbili hawaoni umuhimu wa kulipa posho mbili maana husimamia uchaguzi wa Rais Zanzibar na Wawakilishi na uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge," alihoji.

Akijibu maswali hayo Katambi alisema waraka huo umeanza kutekelezwa na wanazingatia mapendekezo hayo kwa mujibu wa sheria, miongozo na taratibu.

# Shule zina upungufu zaidi walimu 39,000 masomo Sayansi, Hisabati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHULE zinakabiliwa na upungufu wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati 39,610.

Hata hivyo, katika mwaka 2023/24, serikali inategemea kuajiri walimu 12,000 wakiwamo wa masomo ya Hisabati na Sayansi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainab Katimba, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (Chadema), Esther Matiko.

Mbunge huyo alihoji shule za msingi na sekondari zina upungufu wa walimu wangapi katika masomo ya Sayansi na Hesabu.

Akijibu swali hilo, Katimba alisema mahitaji ya walimu wa masomo hayo nchini ni 71,027 waliopo ni 31,417 na upungufu ni 39,610 sawa na asilimia 55.8.

"Serikali inatambua upungufu wa walimu wa masomo ya hisabati na sayansi katika shule za sekondari nchini. kufuatia upungufu huo, serikali imekuwa ikifanya jitihada kila mwaka kuajiri walimu wa masomo mbalimbali wakiwamo wa masomo ya Sayansi na Hisabati," alisema.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2020/21 hadi mwaka 2022/23, serikali iliajiri walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati 10,853.

Matiko alisema Halmashauri ya Tarime ina upungufu wa walimu 83 na kuna walimu wa kujitolea 44 sawa na asilimia 53 na kuhoji kwa kuwa serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 kwanini isitenge asilimia 50 ya ajira kwa wanaojitolea ili kutoa motisha kwa walimu wengi kujitolea na kupunguza uhaba uliopo.

Katimba alijibu kuwa wamechukua maoni ya Mbunge na wataona namna ya kuyachakata kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi kwa kuzingatia miongozo na taratibu za kiutumishi.

Pia, katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti maalum (Chadema), Tunza Malapo, alihoji mkakati wa serikali wa kutatua tatizo upungufu wa masomo ya Sayansi na Fizikia hilo kutokana na utekelezaji wa mtaala wa mafunzo ya amali.

Naibu waziri Katimba alijibu serikali itazingatia katika ajira za walimu wapatikane wa masomo hayo.

Kadhalika, Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson alishauri kuhusu watumishi ikiwamo walimu wanaojitolea, Ofisi ya Rais, Utumishi ilishalieleza Bunge serikali inaandaa mpango maalum kwa ajili yao, TAMISEMI na Utumishi washirikiane ili wapewe kipaumbele kwenye ajira.

## HABARI KASKAZINI



# Uchunguzi dhidi waliochepusha mitaro majitaka waanza

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI inachunguza malalamiko ya baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wanaodaiwa kuchepusha mitaro ya majitaka kwenda kwenye vyanzo vya maji, ambavyo vinavyotegemewa na umma kwa ajili ya huduma ya majisafi na salama.

Kauli kuhusiana na uchunguzi huo ilitolewa jana na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Shaban Mchomvu.

Licha ya kuwepo na Sheria za Usimamizi wa Vyanzo vya Maji, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji kutokana na kuwepo kwa shughuli za binadamu zinazofanyika pasipo kuzingatia sheria zinazosimamia mazingira na rasilimali maji.

"Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayebainika kufanya vitendo vya uharibifu wa mazingira. Tunasikia kila mahali mafuriko, mengine ni ya kujitakia kwa wananchi kuchafua vyanzo vya maji na maji kubadilisha mkondo wake,

"Leo tunafanya usafi kwenye Mto Njoro, kuhamasisha wananchi kujitokeza katika kuhakikisha wanafanya usafi katika maeneo yao na ya vyanzo. Niwaagize wakurugenzi kuhakikisha wanafikisha magari ya kubeba taka kwa wananchi kulingana na siku walizopanga," alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Moshi, Faraji Swai, aliwataka viongozi wa chama kwanzia ngazi ya nyumba kumi hadi wilaya kuwa walinzi wa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya upandaji wa miti kulingana na mazingira husika.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Bonde ya Mto Pangani, Brown Mwangoka, alisema wakati wa usafishaji wa mto huo, walibaini zipo nyumba zinazoelekeza maji taka katika vyanzo vya maji pamoja kutupa taka ambapo aliwataka viongozi wa mtaa, kata na jumuiya za watumia maji kufuatilia kwa kina.

"Hili ni kosa kisheria na tutawachukulia hatua za haraka. Niwaombe wananchi kuacha tabia hiyo kwani madhara yanayoweza kujitokeza ni makubwa ikiwa ni pamoja na kusababisha mlipuko wa magonjwa," alisema Kaimu Mkurugenzi.

Aidha, Makamu Mwenyekiti wa Watumia Maji ya Mto Rau, Habibu Lema, alisema wamekuwa wakihamasisha wananchi kufuata sheria, kanuni na taratibu ya watumia maji pembezoni mwa vyanzo vya maji pamoja na kuwachukulia hatua wanaokiuka.

"Maombi yetu kama jumuiya ni kwa viongozi wa serikali ikiwemo Manispaa ya Moshi kuhakikisha tunapata gari la kuzolea taka kwa wakati ili kuepuka baadhi kutupa taka kwenye vyanzo mara wanapokosa sehemu ya kuhifadhia taka,"alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi, Shedrack Mhagama alizitaka jamii kujifunza tabia ya usafi na kuacha kusubiri sheria.

"Usafi ni tabia, wote inatupaswa kufanya bila kushurutishwa. Anayechafua chanzo cha maji ni yule aliye jirani na chanzo hicho. Pia kunasuala la wapangaji kukaidi kufanya usafi, ni lazima serikali za mitaa kuwajibika na wenye nyumba ili kuleta ufanisi wa kazi," alisema Mhagama.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Fakii Lulandala (wapili kulia), akizungumza na Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Aristidy Raphael kwenye uzinduzi wa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi katika Shule ya Sekondari Mirerani B.W. Mkapa, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC aingilia kati madai waliohama Ngorongoro kutotendewa haki

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

MALALAMIKO ya baadhi ya wafugaji wa jamii ya kimasai waliohama kwa hiari katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kwenda katika makazi mapya ya Msomera, wakidai kutotendewa haki, yamemuibua Mkuu wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, Albert Msando.

Msando, alikutana jana na kufanya mazungumzo na wananchi hao wa Kijiji cha Msomera kilichoko Kata ya Misima, huku akisisitiza serikali haitoruhusu mtu yeyote kufanya vitendo vya utapeli ama udanganyifu katika mpango huo.

"Nimeamua kuja katika kijiji hiki ili kukutana na mwananchi yeyote ambaye anaamini kuwa serikali haijamtendea haki, wakati wa kuhama kutoka ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuja Msomera.

"Nimekuja kusikiliza malalamiko yenu na kutafuta suluhu ya kudumu kama yako madai ya msingi.

"Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya wananchi, ambao wakati wanahama kutoka Ngorongoro kuja Msomera, walikuwa wategemezi katika kaya mbalimbali, ambazo zililipwa stahiki zao zote za mali pamoja na motisha.

..Sasa wako waliojitokeza huko wakidai kuwa wametapeliwa na serikali kitu ambacho si cha kweli. Wananchi 132 ambao waliorodhesha majina yao na kuyaleta kwangu, niliyatuma majina hayo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro."

Msando alisema serikali imegundua kuwa watu hao hawakuwa wakuu wa kaya wakati wanahama.

"Kuna watu wanataka kuleta utapeli katika mpango huu na wengine wapo nchi za nje, wakiamini kwamba kuna fedha za bure ili wafanye utapeli. Jambo hilo halikubaliki," alisema Msando.

Kuhusu wananchi watatu ambao majina yao yameongezeka katika taarifa iliyotolewa na baadhi ya vyombo vya habari, Msando alisema vyombo husika vinafuatilia madai yao, kuona kama yana ukweli.

Wananchi 132 ambao ni wategemezi wa kaya zilizohama kwa hiyari kutoka ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwenda katika Kijiji cha Msomera, waliripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari, wakidai kwamba serikali haijawapa stahiki zao wakati wanahama.

Awamu ya kwanza, serikali ilijenga nyumba 503 katika Kijiji cha Msomera na kuwezesha kaya 551 kuhamia zikiwa na watu 3,010 na mifugo 15,521.

## Wanafunzi MoCU waanzisha klabu kutetea wenye ulemavu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MTAZAMO hasi wa baadhi ya watu kuhusu watu wenye ulemavu bado unatesa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, baada ya kuwapo kwa taarifa za watoto wenye hali hiyo kunyimwa fursa ya kwenda kwenye nyumba za ibada na wengine kufichwa.

Ili kukabiliana na hali hiyo na kuunganisha nguvu na sauti za kundi hilo kwa ajili ya kukemea na kulaani, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), wameanzisha klabu mahususi ya Moshi Co-operative University Students With Special Needs Club.

Jana, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ya Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum, Talky Mohamed, alisema mtizamo huo hasi bado uko wilayani Moshi na unaathiri ustawi na maisha yao katika kupigania haki na fursa sawa kwa kundi hilo.


Ongezeko la wanafunzi hao wa MoCU kutoka 35 hadi 45 kwa mwaka wa masomo 2022/23, ni ishara ya jitihada madhubuti za serikali pamoja na chuo hicho kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa na wanafunzi wengine.

Kutokana na tatizo la jamii hiyo kunyimwa fursa ya ibada, Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo, alisema jamii hiyo licha ya kuwa na ulemavu, lakini si walemavu katika vichwa vyao.

"Niwaambie kwamba watoto hawa ni walemavu, lakini si walemavu katika vichwa vyao. Tuwatie moyo waendelee kumtukuza Mungu, ambaye Mungu ndiye furaha ya mioyo yao," alisema Askofu Dk. Shoo.

Kilio hicho, kimemfanya Makamu Mkuu wa Chuo, Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi MoCU, Dk. Elisifa Nnko, kumwomba Naibu Meya wa Manispaa ya Moshi, Stuart Nathaniel, kwa nafasi yake kuona namna kuisemea jamii ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Alisema: "Ni ombi letu kama jamii ya watu wenye mahitaji maalum hilo ulichukue na pale ambapo mazingira yatakuwa yanaruhusu tafadhali usilihasau kusanyiko hilo la MoCU, kwa kuwa tunajua lina mchango mkubwa katika jamii na katika taifa".



# Kaya 10 zakosa makazi nyumba zao zikibomolewa

**Na Remmy Moka,** SAUT

KAYA zaidi ya 10 zimekosa makazi baada ya uongozi wa Shule ya Sekondari Islamiya iliyopo Mtaa wa Temeke wilayani Ilemela mkoani Mwanza kuvunja nyumba hizo.

Taarifa za awali kutoka shule hiyo zinadai kuwa wanafamilia hao wameshalipwa fidia lakini hawataki kuyaacha makazi hayo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi hao akiwemo Benjamini Njiga alisema mgogoro huo ulianza tangu mwaka 1998 baina ya wanafamilia hao na shule hiyo.

Alisema mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu na ilipofika mwaka 2004 walianza kwenda katika vyombo mbalimbali vya sheria pasipo majibu ya matatizo yao.

Benjamin alisema uongozi wa shule hiyo ulipewa hati kabla ya kuwalipa fidia wanafamilia hao na kwamba kitendo hicho ni cha kitapeli.

Alisema walitoa lawama kwa uongozi uliotoa kibali cha kuvunja nyumba zao pasipo kupewa taarifa, huku kesi yao namba 68/2023 inayohusiana na mgogoro huo ikiwa bado ipo mahakamani.

Alisema kitendo hicho kimewaumiza kwani kimewaacha bila makazi, huku maisha yao yakikosa mwelekeo.

Benjamini aliiomba serikali kuwatazama kwa jicho la tatu ili waweze kupatiwa haki dhidi ya tukio hilo na kuitaka mamlaka inayohusika kufika katika eneo hilo la tukio.

Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, Abdalah Malomo akijibu kwa njia ya simu alikanusha taarifa za uwepo wa mgororo baina ya uongozi wa shule hiyo na wanafamilia hao.

Alisema tayari wameshalipwa fidia zao tangu mwaka 2003 huku akiwatuhumu kutokuwa waaminifu baada ya kulipwa fidia. Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda alisema mgogoro huo anautambua na njia pekee ya kutafuta suluhisho ya suala hilo ni walalamikaji kwenda mahakamani.

Alisema hakuna anayeweza kubadili maamuzi ya Mahakama na bado nafasi wanayo ya kutaka rufaa ili kutafuta haki yao ya msingi, huku akiwataka kwenda katika ofisi ya Wilaya na Mkoa ili kupata ufumbuzi zaidi wa suala hilo.

Alisema endapo ikitokea waliotekeleza uvunjifu wa nyumba hizo walifanya kinyume na utaratibu itawalazimika kuwalipa fidia walalamikaji dhidi ya ualibifu huo

Aidha, aliwataka wananchi kufuata taratibu za kisheria katika kutafuta utatuzi wa migogoro ya ardhi kwani kazi ya wizara ni kusuluhisha migogoro na kutenda haki kwa mtu anayestahili.



Mkuu wa Wilaya ya Serengeti mkoani Mara, Dk. Vincent Mashinji (wa pili kulia), akimsikiliza Mratibu wa Shirika la Worldchanger Vision Tanzania, Sulusi Samwel (kulia), mjini Mugumu juzi, kabla ya kukabidhi vyerahani kwa wahitimu wa fani ya ushonaji katika mahafali ya sita ya Chuo cha World changer Vision, kinachomilikiwa shirika hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TTB yatangaza 'vita' na kampuni zinazowakopa wakulima

**Na Halima Ikunji,** TABORA

BODI ya Tumbaku Tanzania (TTB) imesema itazichukulia hatua kampuni zenye madeni ya msimu uliopita, ikiwa ni pamoja na kutozipa leseni ya ununuzi kwa msimu wa mwaka 2024/25.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa TTB, Stanley Mhozya na kusema kuwa kampuni za ununuzi zinazodaiwa na wakulima wa tumbaku ama ushuru wa halmashauri wanapaswa kukamilisha madeni hayo ili kupata leseni hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema uzalishaji wa tumbaku unaongezeka kila mwaka kutoka kilo milioni 37 kwa mwaka 2023 mpaka kufikia kilo 180 kwa msimu huu.

Alisema mvua ingekuwa ya wastani uzalishaji wa tumbaku nchini ungeweza kufikia kilo milioni 215 zimeshindwa kufikiwa kutokana na mvua kubwa kunyesha kwani wakulima walikuwa wakiweka mbolea inakwenda na maji.

Alisema kufafanua kwamba kutokana na hali ya mvua hiyo ilisababisha mabani mengi ya kukaushia tumbaku kuanguka na hivyo wakulima kukosa kitu cha kukaushia tumbaku yao.

Alisema kwamba tatizo lingine ni ukosefu wa kamba za kufungia tumbaku kuchelewa kuwafikia wakulima kwa wakati na kusababisha zao la tumbaku kukosa ubora hali hiyo ilijitokeza mwaka jana na kwa mwaka huu haitojirudia.

Alisema kampuni za ununuzi wa tumbaku nchini zimeongezeka kutoka tatu hadi kufikia 12 ambazo zilipewa leseni baada ya serikali kuanza kuboresha mazingira mazuri ya uboreshaji ya uwekezaji.

## Wasichana 198,865 kupatiwa chanjo ya saratani Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude amesema wasichana 198,865 wenye umri kuanza miaka 9 hadi 14 mkoani hapa wanatarajia kupewa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi (HPV) ili kukabiliana na ugonjwa huo.

Aliyasema hayo kwenye kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Annamringi Macha.

Alisema utoaji wa chanjo hiyo itakuwa ndani ya wiki moja na itawafikia wasichana 198,865 wenye umri kuanzia miaka 9 hadi 14.

"Utoaji wa chanjo hii ni kuongeza kinga kwa wasichana dhidi ya ugonjwa huo, natoa wito kwa wazazi kuwaruhusu mabinti zao wapate chanjo hii, ili kulinda afya zao na utoaji huu wa chanjo utakuwa endelevu hadi Desemba mwaka huu," alisema Mkude.

Aidha, alitoa maagizo kwa viongozi wa serikali wakiwamo watendaji wa kata na vijiji kuwabaini wasichana ambao hawapo mashuleni ili na wao waweze kupata chanjo hiyo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk.Yudas Ndungile, alisema utoaji wa chanjo hiyo ilianza kutolewa Mwaka 2014 kwa dozi mbili lakini sasa hivi kutokana na mabadiliko itatolewa kwa dozi moja.

Naye Mratibu wa chanjo Mkoa wa Shinyanga, Timothy Sosoma, alisema chanjo hiyo itatolewa kwa shule zote za msingi na sekondari 887 na kwenye vituo vya afya 241.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Paul Julius, aliupongeza Mkoa wa Shinyanga, kutokana na maandalizi mazuri ya utoaji chanjo hiyo baada ya kutembelea baadhi ya maeneo ambapo vitendea kazi vya utoaji chanjo vimeshafika.

## Ugawaji wa taulo za kike wapunguza utoro shuleni

**Na Gwamaka Alipipi**

BAADHI ya wanafunzi na walimu wa shule za sekondari mkoani Geita wamesema ugawaji taulo za kike kwa ajili ya kusitiri wanafunzi wa kike kipindi cha hedhi, umechangia kupunguza utoro wa wanafunzi wanapokuwa kwenye siku za hedhi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti hivi karibuni, wanafunzi na walimu hao walishukuru Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kutatua changamoto hiyo ya usimamizi wa usafi wa hedhi katika shule mbalimbali za mkoa huo.

Walisema tangu GGML ianze ugawaji taulo hizo za kike na kufanya zoezi hilo kuwa endelevu, limebadilisha matokeo ya ufaulu na hata maisha yao.

Mmoja wa wanafunzi hao, Kulwa Lameck ambaye anasoma kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Nyakabale, alisema zoezi hilo limewasaidia kujitambua kutokana na elimu ya afya ya hedhi wanayopatiwa.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Nyankumbu, Rosemary Nicolaus, alisema ameona mabadiliko makubwa katika mahudhurio ya wanafunzi wake na ufaulu wao wa kielimu tangu walipopata mafunzo ya usafi wakati wa hedhi.

Alisema changamoto zinazokabili wasichana wa mkoa wa Geita pia zinawakabili wengine katika mikoa mbalimbali nchini, hivyo ni vema wadau mbalimbali waendelee kuungana mkono dhana ya kutoa misada ya taulo za kike na elimu ya afya ya uzazi kwa wanafunzi wa kike ili waweze kujisitiri na kuondokana na dhana potofu.

Emily Zachariah, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Nyakabale naye alisema; "Sasa najua kuwa hedhi ni sehemu muhimu ya uumbaji kwa wasichana, ni jambo la kawaida na ni sehemu ya maisha yao, linahitaji kuthaminiwa na kuheshimiwa.

Takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF), zinaonesha kuwa kila siku wanawake na wasichana milioni 300 hawana mazingira mazuri ya kujisitiri pindi wanapokuwa kwenye kipindi cha hedhi, hawana yaulo za kike wala elimu ya afya ya uzazi kuhusu usafi wa hedhi.

Shirika hilo linaeleza kuwa kutokana na hali hiyo wanfunzi wa kike hushindwa kuhudhuria darasani kwa siku 40 katika mwaka kutokana na changamoto za hedhi.




**Mbwambo mkono wa 'kielektroniki' unaowagusa watoto waliosahaulika**




Wadau wanapofikiria 'ubatizo wa pili' Chuo Kikuu Dar es Salaam

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 23, 2024
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




**GHF kufichua yaliyofichika darasani ni kupitia vipaji**

ELIMU

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

VIJANA PASUA KICHWA...

# Hawataki ndoa, familia, wala majukumu

## • Utetezi wao; hali ngumu, hatuna hela

TANZANIA ya leo inazo changamoto kuhusu hatima za vijana hasa wa kiume kwa maisha ya sasa na baadaye. Majira yanakwenda, nyakati zinapita na miaka kuongezeka lakini mwelekeo wa vijana wengi siyo wenye kuleta faraja kwenye familia nyingi.

Ikumbukwe tangu mwanzo Mungu aliumba mume na mke, mwanaume akiwa mzaliwa wa kwanza akapewa madaraka ya kuisimamia na kuitunza dunia pamoja na familia, mwanamke akiwa msaidizi maandiko yanaeleza.

Lakini mazingira ya sasa, vijana wa kiume,ingawa siyo wote wamepoteza dira na umuhimu wa kulinda urithi, waliopewa tangu kuumbwa dunia, la kushangaza ni kuona wengi walio na umri wa kuoa waishio mijini na vjijini, wanakwepa kuwa na familia, kuoa au kuzaa watoto. Ukiwadadisi wana jibu jepesi: "hali ya maisha siyo rafiki ". Ni vigumu kwa kijana kuwa na familia hivyo wanasema hawatamani kuoa.

Ni mtazamo hasi unaifanya jamii ipoteze mwelekeo sahihi wa kulitii agizo la Muumba akiwaagiza wanadamu nendeni mkazae, mkaongezeke na kuijaza dunia. Sipati picha kamili maana kujitetea kupitia 'ugumu wa maisha' chanzo chake nini?

Ukiwauliza wapi na vipi wanapohakikishiwa kuwa maisha yatakuwa rahisi au mepesi kula , kunywa, kuvinjari, wanavyotaka bila kutokwa jasho, hawana jibu lakini wanabaki kulalamikia serikali na hata wazazi na walezi kuwa wanatelekezwa. Wengi malalamiko ni hakuna ajira, fedha imekuwa vigumu kupatikana na hawana msaada kutoka kwa jamii.

Vitabu vinaeleza kuwa "kwa jasho lako utakula chakula" na zaidi kuonywa kuwa "asiyetaka kufanyakazi wakati ni mzima wa afya asile chakula". Sasa huo urahisi wa maisha unaingiaje kama siyo kujidanganya na kupelekea kupenya kwa 'roho' haribifu hatimaye kuukumbatia 'uovu' kwa kutaka kujirahisishia maisha?

Mwanamume simama kidete fanyakazi kwa bidii ili uitwe baba wa familia na siyo kinyume chake. Kutaka vya urahisi ni kujidhalilisha na kutothaminiwa vizuri na jamii.

Kwa kukwepa wajibu wa msingi ambao unawataka wanaume wafanyekazi kwa malengo maalumu ili kuifanya Tanzania kuwa na familia lakini pia nchi ikawe na watu wa kutosha. Wakumbuke watu au wananchi ni mtaji muhimu unaohitajika kwa maendeleo ya taifa , bila watu wa kutosha ni kujidanganya na kweli haimo ndani mwetu wakati taifa ni kubwa na idadi ya watu ni ndogo.

Ingawa maeneo mengine hayawezi kukaliwa na watu kama sehemu za ardhioevu, zenye maji na hifadhi za wanyama na misitu, bado idadi ya watu ni ndogo.

Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya 2022 zinaonyesha kuwa idadi ya watu kwa kilometa moja ya mraba (km2) ina wastani wa wakazi 68 . Hata hivyo ipo mikoa ambayo watu ni kidogo kama Katavi wapo 25 kwa km2 au Lindi 18 wakati Ruvuma ni watu 29 kwa km2 moja.

Wakati huo Tanzania Bara inatarajiwa kufikia watu milioni 147 mwaka 2050, kutoka milioni 61 walioko sasa sawa na ongezeko la takribani asilimia 3.2 kwa mwaka.



Wanandoa wakiwa kwenye hafla yao. **PICHA: MTANDAO**

Kwa mwelekeo huo wa vijana kukataa ndoa na kuwa na familia na baadhi kujiingiza kwenye ushoga na usagaji, idadi hiyo itatoka wapi? Labda wahamiaji kutoka nje.

Pamoja na hayo, vijana wa kiume wamekuwa wepesi kukiuka misingi ua ubaba kupitia familia ya mume na mke kuishi pamoja na kuwa na watoto. Unajiuliza kijana mwenye afya njema anachangamkia ushoga na kuona fahari akitangazwa kuwa ni 'shoga' mtaani?

Inawezekana akafanya hivyo kwa tamaa ya kupata fedha haraka kwa kurubuniwa na wenye nia mbaya na kwa kukosa maarifa ya Ki-Mungu anatumbukia kirahisi kwenye mtego wa aina hiyo, lakini mapato ya aina hiyo yana faida gani iwapo hutakuwa na familia?

Vijana wamjue Mungu ipasavyo bila shuruti maana kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa ambayo ndiyo hazina ya mafanikio laa sivyo wengi watajiangamiza kama neno la Mungu linavyoonya: "watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa".

Vijana kumbukeni kukumbatia 'ushoga' ni kutumbukia kwenye dimbwi lililo chukizo kwa muumba wako. Vilevile, ni kuwa na mioyo iliyosheheni mawazo mabaya na kujivika miguu iliyo miepesi kukimbilia dhambi.

Wafahamu kuwa kutumbukia kwenye maovu kama ushoga na kwa kisingizio cha haki za binadamu ni sawa na kukosa maarifa hali inayopelekea maumivu makubwa kwa wazazi na jamii kwa ujumla. Wazazi na walezi wanaposikia au kumshuhudia kijana waliompata akiwa zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ghafla anageuka kuwa mwovu au shoga ni hali tatanishi na isiyohimilika kwao.

Vijana wa kiume na wa kike, jiulizeni ushoga na usagaji una faida kwenu, wazazi, walezi ,jamii na taifa kwa ujumla? Je, mnavutiwa va vitu au vionjo gani mpaka kupagawa kiasi cha kutojali uhalisia wa maumbile yenu? Umezaliwa ni mwanamume iweje uwe na matamanio ya kumuoa mwanamume mwenzako? Kwa vipi uone fahari na kujisifu kuwa umeolewa na mwanamume mwenzako na kujiona ni mke wake?

Binti naye anageuka kuwa mwanamume eti anamuoa binti mwenzake je uhalali huo unatokana na nini? Hakuna cha haki za binadanu wala chochote kile ni uovu uliokithiri mbele za Mungu na aibu kubwa kwenye jamii .

Kwa hili viongozi wa kiroho wa madhehebu mbalimbali simameni imara na kukemea kwa nguvu zote na dunia ielewe kuwa hatuko tayari kukumbatia uovu kwa minajili ya kutaka kufurahisha watu wengine.

Vijana wengi wanalia kuwa hali ya uchumi na maisha ni magumu na ajira ni kidogo kulingana na mahitaji, kazi za kujituma hata kama ni kulima au kazi nyinginezo za kumpatia kijana kipato zinapuuzwa kwa kutaka kupata fedha kirahisi wakati kwa jasho letu; tunapaswa kupata riziki zetu za kila siku.

ELIMU
NA GETRUDE MPEZYA, MOSHI

# Mbwambo; mkono wa kielektroniki unaowagusa watoto waliosahaulika

FREDRICK Mbwambo, ni kijana aliyezaliwa kwenye familia ya kawaida, lakini anayesukumwa na kujali wengine, kuwainua akitumia kidogo alichonacho kuwapa kesho iliyo bora.

Anaamini kumcha Mungu, kumpenda jirani na jitihada binafsi kuwa ndizo silaha za kumfanikisha kufikia popote kuanzia mahala alipo leo na atakapokuwa baadaye.

Mbwambo alipata elimu ya ualimu katika Chuo cha Kinampanda mkoani Singida na kuajiriwa kufundisha katika Shule ya Msingi Nyamadoke iliyoko Sengerema anakoanzia kazi ya kushika chaki darasani.

Anafanyakazi kwa muda na kujiendeleza zaidi, akisoma hadi kidato cha sita na kujiunga na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na kwa sasa ni mwanafunzi wa kozi ya uhusiano wa kimataifa na diplomasia jijini Arusha.

Anaamini kuwa ni lazima kujituma, kujitolea na kutumikia jamii. Leo Mbwambo amejitwisha majukumu muhimu, baada ya kuanzisha Taasisi ya Gentech Foundation inayojihusisha na ustawi na kutoa elimu ya teknolojia, vifaa kama vile kompyuta za mezani na mpakato na vishikwambi (tablets) kuwawawezesha watoto wasio na uwezo kujifunza sambamba na kuwapatia vifaa vya michezo kama mipira na jezi ili washiriki michezo.

Amewafikia watoto kwenye baadhi ya shule ikiwamo Shule ya Msingi Kijenge, Sekondari ya Olorieni na kituo cha watoto yatima cha Moses Comfort cha USA River Arusha.

Lakini, pamoja na kuwafikia walio shuleni hajawasahau wanaoishi kwenye mazingira magumu hasa wanaokaa mitaani. Ameanzisha program maalumu za kuwaagusa za 'TechAkid na TechAkidToCode akiwafundisha masuala ya kimaisha, teknolojia za kielektroniki, vifaa vyake ili wazitumie ziwasaidie, maarifa na stadi mbalimbali kuwakwamua na kuwawezesha kuzisaidia pia jamii zao.

Mbwambo anapozungumza na Nipashe anaeleza kuwa anatumia nguvu, mali na juhudi binafsi, vifaa, fedha na michango ya wadau mbalimbali kufanikisha mikakati hayo na mafunzo kwa watoto anaoamini ni nguzo muhimu


Fredrick Mbwambo, (kulia) katika moja ya mikusanyiko ya kijamii. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

> Mwaka 2020 niligombea ubunge jimbo la Same Magharibi kutokana na mazingira ya kisiasa wakati ule, nilifukuzwa chuoni, familia yangu ilikata tamaa na waliacha kutoa msaada.

kwa maendeleo ya nchi.

"Mpaka sasa tumewafikia watoto zaidi ya 500. Lengo la Gentech nikuwahudumia watoto masikini wasio na uwezo wa kupata elimu wala vifaa vya kiteknolojia ili kupunguza pengo la kidijitali kati ya watoto wa familia za wenye nacho na wasio nacho." Anasema Mbwambo.

Anaeleza kuwa hayuko peke yake anashirikiana na Adam Malick mwanzilishi mwenza wa taasisi ya Gentech. Akiwa mtaalamu wa TEHAMA na kwamba ni mshiriki muhimu kwenye kutimiza azma hiyo, akiandaa mitaala, na vifaa sahihi vya kujifunzia na kufundishia pamoja na kuwa na matumizi chanya na yenye tija ya teknolojia kwa watoto hao.

Mbwambo anawakilisha matumaini na ujasiri kwa vizazi vijavyo, mtu anayeweza kuitwa kijana wa mfano wa kuigwa na kielelezo cha mabadiliko katika jamii anayewafundisha vijana kujitoa kwa ajili ya wengine kwa manufaa ya taifa letu.

## MAISHA NI KUJARIBU

"Mwaka 2020 niligombea ubunge jimbo la Same Magharibi kutokana na mazingira ya kisiasa wakati ule, nilifukuzwa chuoni, familia yangu ilikata tamaa na waliacha kutoa msaada. Nilibakia mwenyewe na "imani" yangu ya kumcha Mungu, kumpenda jirani na jitihada binafsi nilisimama. Sikuwa na fedha wala marafiki wakunisaidia katika maono yangu ila niliona kuwa ni lazima kujaribu na huko ndiko kuweza."

Anasema alipata nafasi ya kwenda Misri lakini fedha ikawa kikwazo kikuu."Safari yangu ya masomoni Misri nilikwenda kwa msaada wa kanisa. Nauli nililipiwa na Mchungaji kanisani, Pastor Orche Mgonja wa kanisa la Lift Him up. Alinikopesha Shilingi million 1.5 ili nihudhurie mafunzo ya uongozi chini humo.

Nilipofika kule nilikutana na viongozi mbalimbali, akiwemo Balozi wa Tanzania Misri wakati huo Dk.Emmanuel Nchimbi."

Alikwenda kujifunza mafunzo ya uongozi chini ya Programu ya Rais wa Misri, Abdel Fatah El-Sis, na kutunukiwa cheti na nishani ya heshima. Alipewa pia fursa ya kutembelea Bunge Misri, Chuo cha Polisi (Accademy), alizuru mfereji wa Suez (suez Canal), mji mkongwe wa Alexandria na Makumbusho ya Taifa kujifunza zaidi kuhusu historia ya kiungozi tangu kale mpaka sasa.

Mbwambo anamtaja Katibu Mkuu wa CCM Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, kuwa ana nafasi katika maisha yake na amechangia kupata mafanikio, akieleza alivyomsaidia akiwa nchini Misri kwenye masomo

"Baada ya mafunzo mimi na mwenzangu mmoja tukijijua hali zetu, tulishauriana tuutafute Ubalozi wa Tanzania tupate hifadhi siku mbili. Cha ajabu hata hatujafanya hivyo Balozi Dk. Nchimbi akatualika nyumbani kwake na tukakaa kwa siku mbili, alitupa fedha ili tununue zawadi, alitoa gari la ubalozi lituhudumie na asubuhi siku ya safari tulipelekwa uwanja wa ndege kwa heshima. Matendo hayo yote kwangu yalikuwa ushuhuda wa imani yangu na namna Mungu anavyoweza kuinua watu wakunisaidia katika mambo mbalimbali."

Balozi Nchimbi sikumfahamu kabla, sikuwahi hata kumuona lakini Mungu alimuinua akanitendea yote haya. Nami naamini nina deni la kuwatendea wengine mema kwa kuwapa elimu kama ambavyo mimi nimeshikwa mkono na wengine, anaeleza kijana huyo.

## TUSIKWEPE SIASA

Mbwambo anaamini kuwa siasa si jambo la kukwepa. Ni kila kitu ndiyo inayoanzisha na kutunga sheria zote akimaanisha kazi za wabunge Dodoma na wawakilishi visiwani Zanzibar. Kwa kuthibitisha hilo anasema ndiyo maana ni mwanachama wa CHADEMA, tangu mwaka 2008, na katika uchaguzi mkuu wa 2020 aligombea ubunge jimboni Same Magharibi.

Ingawa hakufanikiwa katika kura za maoni, anaeleza kuwa alimuunga mkono mgombea wa chama hicho Gervas Mgonja, na kuwa meneja wa kampeni yake.

Anawahimiza vijana kuacha mijadala ya kandanda na kukaa vijiweni bali waangalie maendeleo na kupenda kujiingiza kwenye masuala ya ubunifu, kujituma , uongozi, mijadala na kuibua fikra tunduizi (critical thinking) ili kupata mawazo yanayobadili maisha yao.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Wadau wanapofikiria 'ubatizo wa pili' Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

• Hoja ni kumkumbuka mwanamama muasisi na mbeba maono



Mwami Tereza Ntare, enzi za uhai wake. **PICHA: MWANDISHI WETU**

TEREZA Joseph Ntare aliyezaliwa 1927 na kufariki 1990, maarufu kama Mwami Tereza Ntare II ni mwanamama nguli, aliyefanya makubwa kwa taifa hili, lakini wengi hawamfahamu.

Aidha, alikuwa mhifadhi mkuu wa jamii, mila na desturi, uongozi bora na mpiganaji, Chifu Mkuu mwanamke wa kwanza akiongoza machifu wote wa Tanganyika wakati wa ukoloni wa Muingereza.

Akitajwa kuwa mwanamama aliyeruka viunzi na kuukabili mfumo dume na ukosefu wa usawa wa kijinsia, akipaa kama 'tai, kuleta mawindo ya ushindi kwenye majukumu yote aliyokuwa akiyasimamia, inasikitisha kuwa hafahamiki na wengi.

Kwa kuona upungufu huo, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa kushirikiana na Mtandao wa Ke-Storia, Makumbusho ya Taifa na familia ya Mwami Tereza , unaandaa jukwaa la kusherehekea mafanikio yake.

Mengi yanazungumzwa kwenye maadhimisho yake, yanayofanyika kwenye Makumbusho ya Taifa Dar es Salaam mapema mwezi huu.

Anasifiwa kwa jinsi alivyofanikisha kupatikana uhuru mwaka 1961, kando na hilo ujasiri, kuwa na fikra zilizopevuka, kuona mbali na kutambua vipaumbele kunampa heshima ya kuwa mama aliyeota na kuitimiza ndoto ya kuanzishwa Chuo Kikuu -UDSM.

Ni maelezo ya meja mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Minaeli-Hosana Mdundo, anayeieleza hadhara ya washiriki wa mafanikio ya Mwami Tereza yakihusisha wanafamilia, asasi za kiraia, watendaji wa serikali.

"Katika Mkutano Mkuu wa TANU uliofanyika Tabora mwaka 1958 pamoja na ajenda mbalimbali, mojawapo ni ujenzi wa chuo kikuu cha Tanganyika.

Mwami Tereza, alikuwa mjumbe wa mkutano huo na akawa miongoni mwa waliopewa jukumu la kufanikisha kujengwa chuo hicho." Anasema Minaeli.

Minaeli mtunza nyaraka za zamani (archivist) mstaafu, anatoa ushuhuda huo na kueleza kuwa chuo kikuu cha UDSM kilianza miezi michache kabla ya uhuru na Mwami Tereza ni mbeba maono.

Katika kusanyiko hilo wengi wakatafakari jinsi mwanamama huyu alivyoshiriki kuanzisha UDSM na kuhoji hivi hakikustahili kupewa jina Lake?

Moja ya mabweni katika chuo hicho yana jina la Dag Hammarskjöld, (Hamaskod) Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, aliyeuawa 1961 katika ajali ya hekopta akiwa kwenye misheni ya kusaka amani ya Congo.

Ni ujumbe kwa serikali kumuenzi mwanamama huyo mashuhuri, shujaa na aliyekuwa na bidii ya kujenga Tanzania yenye maisha bora kwa kila mmoja kwa kuiita UDSM Chuo Kikuu cha Mwami Tereza Ntare II.

**KUWASAHAU KINAMAMA**

Maadhimisho ya mafanikio ya Mwami Tereza, yanagundua kuwa wanawake wamefanya mengi lakini hawaonekani katika uandishi wa historia.

Profesa Ruth Meena, kutoka Mtandao wa KE-Storia, (Her Story), unaotetea haki za wanawake, kuziibua na kuziandika upya kwa usahihi kwa kuonyesha mafanikio, anasema licha ya Mwami Tereza kufanya makubwa historia yake haifahamiki tena inasahaulika.

Anasisitiza kuandika na kuweka uwiano sawia (balanced story) ya wote waliochangia maendeleo na mafanikio ya Tanzania.

Anaongeza kuwa ni wakati wa kuachana na mtindo wa kuandika taarifa zinazoonyesha upande mmoja na kuupuza mwingine hasa wa wanawake.

Anashauri kurekebisha historia, kumbukumbu na taarifa zote zilizoandikwa kwa upendeleo wa upande mmoja na kubagua kundi jingine ambalo pia limechangia mafanikio ya taifa katika nafasi mbalimbali.

"Jukumu la kurekebisha kumbukumbu na taarifa hizo au kuzikomboa upya zilizopotoshwa lisiachiwe familia bali serikali iongoze masahihisho ya mambo yote yaliyowaondoa wanawake katika mapambano ya ukombozi wa taifa,"anasema Profesa Ruth.

Anaongeza zaidi: "Vitu vyote vilivyoporwa na wakoloni hasa vichwa vya wapigania uhuru wawe wanawake au wanaume, serikali isimamie kuvidai na kuvirudisha isiziachie familia kuvidai."

Akizungumza mbele ya Waziri wa Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, Prof Ruth, anasema inashangaza Makumbusho ya Taifa kwa miaka mingi haikuwa na picha ya mwanamke na kusema ni wakati wa kufanya mabadiliko.

Anasema ni mambo yaliyoanzishwa na kupotoshwa na wakoloni lakini wakati umefika yasahihishwe ili kuweka uwiano sawa wa wanawake na wanaume waliochangia kufikisha Tanzania hapa ilipo leo.

**MAKUMBUSHO KIGOMA**

Waziri Ndumbaro, akizungumza katika maadhimisho hayo, anaahidi serikali itajenga Makumbusho ya Mwami Tereza Kigoma kuenzi kazi zake na michango mbalimbali ya wanawake walioshiriki katika harakati za ukombozi na maendeleo ya Tanzania.

> Katika Mkutano Mkuu wa TANU uliofanyika Tabora mwaka 1958 pamoja na ajenda mbalimbali, mojawapo ni ujenzi wa chuo kikuu cha Tanganyika.

Anasema makumbusho ya Mwami Tereza yatahifadhi historia sahihi itakayokuwa imeandikwa na Watanzania wenyewe.

Anatangaza kuwa kuanzia sasa kila Machi 8 Siku ya Wanawake Duniani, itakuwa siku ya kuadhimisha na kumuenzi Mwami Tereza Ntare II.

Agnes Shinganya mjukuu wa Mwami Tereza, akizungumza kwa niaba ya familia anasema ni dhamira ya muda mrefu ya familia ya Mwami kumuenzi kiongozi huyo baada ya kuona historia yake, inasahaulika na inapotoshwa.

Anasema wameazimia kuanzisha Makumbusho ya Mwami mkoani Kigoma ili kuendelea kuhifadhi historia ya kiongozi huyo wa jamii wa watu wa eneo la Heru juu, aliokuwa anawaongoza.

Anaamini Makumbusho hayo ni chanzo cha mafanikio kiutafiti, utalii na kuchangia maendeleo ya elimu.

**KURUDISHA FUVU ZA ZINJI**

Joseph Macha, Kaimu Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni, anasema taasisi hiyo inamuenzi Mwami Tereza kwa mambo makubwa aliyolifanyia taifa ikiwamo kurudisha fuvu la binadamu wa kale Zinjanthropus kutoka Ulaya, akiwa mjumbe wa bodi.

Fuvu hilo ni la binadamu wa kwanza lilinalokadiriwa kuwa na umri wa miaka milioni 1.75 iliyopita lililogunduliwa mwaka 1959 na wanaakiolojia Mary na Louis Leakey katika Bonde la Olduvai Gorge mkoani Arusha.

Macha anaongeza kuwa makumbusho hiyo imekusanya na kuweka taarifa za historia ya Mwami Tereza na kwamba yapo mengi anayokumbukwa kuyasimamia kwa mafanikio.

"Amekuwa chifu kiongozi wa machifu wote Tanzania, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, mjumbe wa bodi ya Makumbusho ya Taifa.

Anaahidi kushirikiana na wadau mbalimbali katika kufanya utafiti na kukusanya kumbukumbu zitakazofanikisha kuanzishwa Makumbusho ya Mwami Tereza kuenzi historia na mafanikio aliyoliachia taifa.

ELIMU
NA GWAMAKA ALIPIPI

# GHF kufichua yaliyofichika darasani kwa kupitia vipaji

VIJANA kukosa ajira ni janga pasua kichwa likigusa karibu mataifa yote, lakini tatizo ni kubwa zaidi katika mataifa maskini ikiwamo Tanzania.

Taasisi ya Great Hope Foundation (GHF) ya Dar es Salaam, imeliona hilo na kujitosa kulikabili, ikianzisha tuzo za Uwezo Award, kuhamasisha utambuzi wa vipaji na uwezo wa wanafunzi shuleni.

Mratibu wa tuzo hizo, Noelle Mahuvi, anazungumza na Nipashe, jijini Dar es Salaam, akieleza nia ya kuwafikirisha vijana wadogo waliopo shuleni ili watambue uwezo wa ziada, wajue namna wanavyoweza kuishi na kufikia malengo na ndoto zao wanapomaliza masomo.

Ikumbukwe wanaolia kukosa ajira ni makundi yote, wasomi na wasiosoma kutokana na sababu mbalimbali. Ila kwa wenye elimu kuna kitu wanakimudu nje ya taaluma yao ila inaonekana hawakukitambua mapema, anasema Noelle.

Kimbilio la wengi hivi sasa ni shughuli za kujiajiri, hata hivyo kwa Tanzania wanafunzi bado wanaendelea kusoma elimu iliyo vitabuni inayodaiwa kwa kiwango kikubwa haiwapi stadi za kujiajiri.

Kutokana na kutambua uwezo wa watoto nje ya masomo ya darasani, Noelle anasema maono ya GHF ni kujenga kizazi kipya kilichowezeshwa, kilichoendelezwa na chenye kuwajibika kinachoweza kuleta mabadiliko kupitia vipaji na ubunifu.


Anataka kuwa na kizazi chenye mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa na kuondoka na kile kinachojaa unyonge kutokana na kutojua hatma yake.

"Tunaamini vijana wana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii endapo, watawekewa majukwaa yatakayowasaidia kuelewa na kutumia uwezo wao kikamilifu," anasema Noelle.

Anasema GHF itaendelea kutekeleza programu za kibunifu, ambazo zinawasaidia vijana kupata ujuzi unaofaa ambao unaweza kuwasaidia kustawi katika soko la ajira kupitia kujiajiri au kuajirika kwa urahisi.

**UJIO UWEZO AWARD**

Noelle anasema Uwezo Programu ilianzishwa mwaka 2016 kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wa shule za sekondari kujifunza na kuonesha uwezo wao ambao hauonekani kwa urahisi wakiwa darasani.




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibiti, wakisherehekea ushindi baada ya kupata hundi. **PICHA: GHF**

> "Tunaamini vijana wana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii endapo, watawekewa majukwaa yatakayowasaidia kuelewa na kutumia uwezo wao kikamilifu.

Anafafanua kuwa programu hiyo imejikita kuwapa wanafunzi jukwaa la kujifunza ujuzi wa kijasiriamali wa karne ya 21, ukihusisha ubunifu, kujiamini, uongozi na kutatua changamoto na kukabiliana na changamoto za soko la ajira, kujiajiri au kuajirika kwa urahisi.

Noelle anasema wanafunzi wanufaika wa programu hiyo wamekuwa wakifanya vizuri katika maeneo mbalimbali baada ya kumaliza shule.

Anasema baadhi yao wamefanikiwa kufungua asasi za kijamii, na wengine wanafanya biashara zinazowaingizia kipato kikubwa na kumudu maisha yao na familia zao.

Kwa mujibu wa Noelle programu ya uwezo ilianza ikiwa na mradi mmoja wa Uwezo Award mwaka 2016 ukizifikia shule 20 na mpaka sasa programu ina miradi minne na shule 250 zinanufaika kwa mwaka. Anaitaja miradi hiyo kuwa ni Uwezo Award, Uwezo Bonanza, Uwezo Kinara na Uwezo Klabu.

Kupitia Uwezo Award, wanafunzi hujifunza kwa kutatua changamoto zilizopo kwenye mazingira yao wakitakiwa kubuni na kutekeleza miradi ya kijasiriamali ambayo itatatua changamoto hizo.

Hutakiwa kuwa na vigezo vikuu vitatu, kwanza mradi wanaoutekeleza uwape fursa ya kutambua na kutumia vipaji vyao iwe kuimba, kuchora, kucheza, pili uwape fursa ya kujifunza ujuzi mpya kuuza, ufundi na tatu mradi huo ulete matokeo chanya kwenye jamii, anasema.

Miradi bora hutambuliwa kwa kupewa tuzo na shirika kila mwaka, kwamba tangu mwaka 2016 mpango huo umewafikia wanafunzi takribani 1,200 walioko kwenye shule zaidi ya 5,000 na za mikoa ya Dar es salaam, Pwani na Morogoro, anasema.

Mratibu wa tuzo anasema mwaka 2023 sekondari tatu bora za juu za mkoani Pwani zilizoshindania tuzo za dhahabu, nazo ni Kibiti mshindi wake akipata tuzo ya dhahabu na Sh. 1000,000.

Nyingine ni Sekondari ya Kibaha washindi wawili walipata Sh. 500,000 wakati Victory washindi watatu walipata tuzo ya Sh.300,000.

**WANUFAIKA WAELEZA**

Sarah Petro, mhitimu katika Sekondari ya Kurasini mwaka 2019 ambaye kwa sasa ni mjasiriamali anayetengeneza keki, karanga, ubuyu na pipi anasema ujuzi wa kutengeneza bidhaa hizo aliupata akiwa shuleni kupitia Uwezo Award.

Anasema akiwa mwanafunzi alishiriki mashindano yaliyoandaliwa na GHF kupitia Uwezo Award na kwamba kwa kushirikiana na wanafunzi wenzake walilima mboga, walitengeneza karanga, ubuyu na pipi

"Fedha tulizozipata tulizitumia kwa kutembelea watoto yatima. Lakini kwa sasa ni mjasirimali ujuzi niliupata ujuzi nikiwa shuleni, ile miradi iliniwezesha nisiwe muoga, niwe kjasiri na siogopi nikikosea," anasema Sarah.

Omary Baajun, mhitimu wa Shule ya Sekondari Mugabe mwaka 2016 kwa sasa ni mjasiriamali wa kuzalisha vitabu na vipeperushi anasema akiwa shuleni alishiriki mradi wa Uwezo Award akishirikiana na wenzake kwa kutengeneza mazuria ya vitambaa.

"Tulikuwa tunaokota vitambaa kwa mafundi cherehani mitaani, tulitengeneza mazuria na kuwauzia walimu. Pia tulianzisha shamba na kulima bamia, mboga na kunde. Kusema ukweli hivi sasa nalima pia nimejiajiri," anasema Baajun.

Boaz Peter, mwanafunzi wa Tambaza Sekondari ya Dar es Salaam anasema ameshiriki tuzo za Uwezo Award mwaka jana kipengele cha mwimbaji bora wa kiume na kushika nafasi ya kwanza. Anasema mashindano hayo yaishirikisha shule zaidi ya 20 za Dar es Salaam.

"Hii Programu ya Uwezo Award kupitia Tuzo za Uwezo Award zimenisaidia .Zimeniwezesha kusafiri kimataifa kwenda Rwanda na kushiriki matamasha mbalimbali. Pia zimeniwezesha kuimba katika matamasha ya Benki ya NMB na NBC, maadhimisho ya kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere niliweza kuimba. Pia Julai mwaka huu ninatajia Kwenda Liberia kuhudhuria mkutano wa Pan-Africanism" anasema Boaz.

Nancy Fausten kutoka Sekondari Zanaki mwaka 2020, kwa sasa ni mwasisi na mkurugenzi wa taasisi iitwayo binti hodari anasema akiwa shuleni alishiriki mradi wa kukarabati vyoo vya shule pamoja na mgahawa kupitia Programu ya Uwezo Award.

"Nilishiriki mara mbili, kwanza nikiwa kidato cha tano na pili nikiwa kidato cha sita. Tulishika nafasi ya pili kimkoa. Tulitengeneza shanga za mkononi na kuuza mtaani.Tuliandaa shughuli ya vipaji suleni. Pesa tulizozipata tulizitumia kukarabati vyoo na mgahawa wa shule," anasema Nancy.

Anasema kikundi chao kilishika nafasi ya kwanza katika Tuzo za Uwezo Award mkoa wa Dar es Salaam ikishirikisha zaidi ya shule 100. Anasema walipewa zawadi ya Sh. 500,000 pamoja na kutembelea mbuga ya wanyama.

Nancy anasema akiwa shuleni walianzisha kikundi walichokiita vikio ambacho kilikuwa kinafanya miradi ya kusaidia jamii ikiwemo kuwatembelea wenye mahitaji.

Anabainisha kuwa kupitia Program ya Uwezo amepata faida nyingi kimaisha mojawapo ni ujuzi wa kuwa kiongozi ambapo kwa sasa ameanzisha taasisi na kuwaongoza watumishi zaidi ya 10.

Anasema pia imemjengea uwezo wa kutatua matatizo na moyo wa kujitolea.



## Jafo: Bila elimu hatuwezi kufikia uchumi wa viwanda

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo amesema Tanzania haiwezi kufikia lengo la kuwa nchi ya uchumi wa viwanda kama haitawekeza kweye elimu.

Alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na wazazi na wanafunzi kwenye mahafali ya kwanza ya kidato cha sita na uzinduzi wa maabara ya kisasa ya masomo ya sayansi katika Shule ya Sekondari ya Fountaine Gate ya jijini Dodoma.

Alisema ili kufikia azma ya uchumi ya viwanda kama taifa linapaswa kuwekeza katika sekta ya elimu ili kupata rasilimali watu ya kutosha, ili kuwatumia katika viwanda vitakavyo anzishwa nchini.

“Hatuwezi kufikia azma ya kuwa na taifa la uchumi wa viwanda kama hatutawekeza kwenye elimu, ndiyo maana serikali imeweka jitihada katika uwekezaji kwenye sekta ya elimu kujenga madarasa, nyumba za walimu na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji katika sekta ya elimu” alisema.

Aidha, aliipongeza shule hiyo kwa kuanza kutoa masomo kwa kutumia tahasusi mpya ambazo zinajikita katika masuala ya uhifadhi wa kimazingira ili kukabiliana na atahri za mabadiliko tabianchi.

Jafo alisema hali hiyo itasaidia Watanzania kuwa na uelewa mpana wa athari zitokanazo na mabadiliko tabianchi na kukabiliana nazo kwa kutunza mazingira.

Mkuu wa Shule ya Fountaine Gate Dodoma, Spicious France alisema shule hiyo inawalea wanafunzi kufuata misingi mitatu ambayo ni maarifa, hekima na vipaji.

Alisema: “Mheshimiwa katika eneo la maarifa shule imefanikiwa kufanya vizuri kwenye mitihani ya ngazi mkoa kwa kushikia nafasi ya tatu kiwilaya na nafasi ya tano kimkoa katika mitihani ya utimilifu kwa mwaka wa masomo 2023/2024, malengo yetu ni kuhakikisha kila mwafunzi wa kidato sita anapata daraja kwa kwanza katika mtihani wa taifa utakao anaza Mei 6, mwaka huu”.

# Dk. Gwajima awatwisha ‘zigo’ MEWATA elimu ukatili kijinsia

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na wenye Mahitaji Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wanachama wa Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), kutoa elimu kwa jamii kuhusiu masuala ya ukatili wa kijinsia, hususani ukekataji kwa watoto.

Alitoa agizo hilo wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 21 wa MEWATA, unaofanyika kila mwaka.

Dk. Gwajima alisema jambo la muhimu hivi sasa ni kuwafikia wananchi hususani vijijini ambapo idadi kubwa inaonyesha wengi wao hawapati elimu ya ukatili wa kijinsia.

Alisema zipo baadhi ya sehemu hapa nchini bado wanaendelea kuwakeketa watoto wakike bila kujali madhara yanayoweza kuwapata mabinti hao na kumsababisha kupoteza uhai na hata kukatisha ndoto zao.

Kadhalika, alitaja takwimu za ujumla kupitia Ofisi ya Takwimu ya Utafiti wa Demografia na Afya 2015-2016, zinaonyesha kuwa asilimia 40 ya wanawake wenye umri wa miaka kati ya 15-49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili na asilimia 17 ya wanawake wamefanyiwa ukatili wa kijinsia.

Alisema jamii bado inakabiliwa na changamoto ya mila na desturi kandamizi ambazo zinazowazuia wanawake na watoto kufikia ndoto zao na kutoa mchango wao katika ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

Dk. Gwajima aliwasihi wanachama wa chama hicho kutokuwa na aibu pindi wanapopata migogoro yoyote itakayowasilishwa, pamoja na kuwaeleza wawazi tatizo ni nini ili kusaidia kulitatua mapema.

Rais wa MEWATA, Dk. Zaitun Bhokhary, alimpongeza Dk. Gwajima kwa ushirikiano alioutoa na kuahidi kuwa watamtembelea ofisini kuhakikisha wanaingia mkataba utakaosaidia afya ya mama na watoto.

Akitaja kauli mbiu ya mkutano huo kuwa ‘tushirikiane kutoa kipaumbele kwa afya ya wanawake na watoto kwa ustawi wa jamii’ ikiwa na lengo kubwa la kukuza mshikamano na uhusiano katika kuhimiza na kukuza utafiti wa kuboresha huduma ya afya kwa wanawake na watoto.

Makamu wa Rais MEWATA, Dk. Marry Mwanyika, alisema wapo tayari kutoa elimu kwa jamii na kuangalia namna nzuri ya kuweza kuondoa masuala ya ukatili wa kijinsia unaoendelea katika baadhi ya sehemu nchini.

Mratibu wa Kamati ya Haki za afya ya uzazi, kutoka Chuo Kikuu Cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS), Emmanuela Maira, alisema wataandaa jarida litakalobeba maudhui mbalimbali ya kuielimisha jamii na masuala ya ukatili wa kijinsia.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na wenye Ulemavu, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza katika Mkutano wa 36 wa Chama cha Wanawake Madaktari Tanzania (MEWATA), jijini Dar es Salaam jana, wenye kauli mbiu ya “tushirikiane kutoa kipaumbele kwa ajili wanawake na watoto kwa ajili ya ustawi wa jamii”. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Uchaguzi wa wafugaji wafutwa kisa ukiukwaji wa Katiba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME Huru ya Uchaguzi ya Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) imebatilisha na kufuta matokeo ya uchaguzi ngazi ya taifa katika Wilaya za Songwe, Mbarali na Igunga kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uvunjifu wa Katiba.

Mwenyekiti wa CCWT, Charles Malagwa alitoa tamko hilo jana jijini hapa, alipokuwa akitoa maadhimio ya kikao kilichoketi Aprili 16 mwaka huu cha kujadili na kutoa maamuzi juu ya malalamiko na rufaa mbalimbali za wanachama waliokuwa wagombea wa nafasi za wilaya kanda na kitaifa.

“Uchaguzi huu ulifanyik Aprili 8, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma chini ya Kifungu cha 45, 46 na 48 cha kanuni za uchaguzi za chama. Tume imefikia uamuzi wa mwisho wa kubatilisha na kufuta matokeo yote ya kitaifa, Kanda za Kusini na Kati katika Wilaya ya Songwe, Mbarali na Igunga na uchaguzi tajwa utapangiwa tarehe nyingine na mchakato kuanza upya” alisema Malangwa.

Malangwa alisema uchaguzi huo uligubikwa na uvunjifu wa Katiba ya Chama cha Wafugaji Tanzania ya mwaka 2013 Toleo la Mwaka 2023 Sehemu ya Nne Ibara ya 2.0 ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 33,34 (2),35(1-6),36 (1-5), 43(1(ii) na 47 (9),(11) na (13) ya Kanuni za Uchaguzi.

Alisema pia kulifanyika kampeni za mabango na vipeperushi vya mgombea nafasi ya mwenyekiti Mrida Mshota Marocha na mgombea nafasi ya Katibu Mkuu Mathayo Daniel Mgusa ndani ya ukumbi wa mikutano wa uchaguzi kinyume na Kanuni ya 34 (2) na 43 (1(ii).

Aidha, alisema daftari la wapiga kura kutozingatiwa kinyume na Kanuni ya 36 (1-5), wajumbe waliohudhuria ukumbini na kupiga kura ni mara mbili zaidi ya wajumbe halali wa mkutano mkuu wa chama chini ya Ibara ya 3.3 Sehemu ya 5 ya Katiba.

## RC atangaza ‘vita’ na wanafunzi wanaopata ujauzito

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego amesema mwanafunzi yeyote atakayebainika kupata ujauzito atakuwa wa kwanza kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria kabla ya aliyempa ujauzito.

Alitoa kauli hiyo juzi katika ziara yake ya kikazi ya siku mbili katika Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni, wakati akikagua ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Dendego alisema kuna tatizo kubwa la watoto wa kike ambao ni wanafunzi kupewa ujauzito na hivyo kukatisha masomo na kwamba ili kukomesha tatizo hilo ni kuanza kukamata msichana aliyepata ujauzito na baadaye mvulana ambaye atakuwa mtuhumiwa namba mbili.

Dendego alisema: “Nikikuta msichana umepata ujauzito wewe utakuwa mshtakiwa namba moja na wewe ndiye utakayeenda jela bila huruma na tumbo lako utajifungulia huko huko.

Kwa sababu mna tabia ya ukipata mimba tunaenda kukimbizana na mtoto wa kiume si sawa wote mlishirikiana kwa hivyo yeye atakuwa mshtakiwa namba mbili na msichana atakuwa mshtakiwa namba moja”.

Kuhusu wanafunzi 4,000 ambao hawajaripoti shuleni hadi sasa alitoa muda wa mwezi mmoja kwa makatibu tarafa na maofisa watendaji wa vijiji na kata wahakikishe wanawasaka na kuwarudisha shuleni.

Alisema itakuwa jambo la aibu kwa Serikali kujenga shule kwa gharama kubwa, huku wanafunzi wanaotakiwa kusoma kwenye shule hizo hawapo.

Aidha, aliagiza kupatiwa taarifa zote za wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambao hawajaripoti shuleni mpaka sasa, hata kama wamehama na shule walipohamia ili aweze kufuatilia.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida Dk. Fatuma Mganga, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kitaraka iliyopo katika Halmashauri ya Itigi baada ya kukagua ujenzi wa nyumba za walimu aliwataka wanafunzi kusoma kwa bidii na kuwa mfano kwa wazazi.





# Mafuriko yasababisha wananchi Kata 13 kukosa makazi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

KATA 13 katika Halmashauri ya Kyela mkoani Mbeya, zimeathirika na mafuriko huku baadhi ya maeneo nyumba zikibomoka na zingine kuzingirwa na maji hali iliyosababisha wananchi kukosa makazi.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase aliyasema hayo wakati wa kupokea misaada kwa waathirika wa mafuriko hayo iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alizitaja baadhi ya kata zilizoathirika kuwa ni Katumba Songwe, Mwaya, Ngonga, Kanjunjumele, Bujonde, Lusungo na Ndobo na kwamba baadhi ya kata hizo zimeathiriwa na mafuriko ya mito na baadhi zimeathiriwa na kujaa kwa Ziwa Nyasa.

Alisema mafuriko hayo yamesababishwa na mvua ambayo imenyesha mfululizo katika Wilaya ya Rungwe na kwamba kwa wilaya hiyo mvua inayonyesha ni ya kawaida.

"Mvua hii hainyeshi kwenye wilaya yetu, inanyesha kwenye wilaya nyingine hasa Rungwe na Ileje ambazo zote zipo kwenye miinuko na maji yake yanashuka huku, lakini kata iliyoathirika zaidi ni Mwaya," alisema Manase.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwaya ambayo nayo iliyoathirika zaidi na mafuriko hayo, Venuster Mpogole alisema kata yake ina vijiji 10 na vitongoji 32 na kwamba vijiji vyote vimevamiwa na mafuriko hayo.

Alisema mafuriko hayo yalitokana na kutapika kwa Mto Rufilyo na Mto Mbaka ambayo yote vyanzo vyake ni katika Wilaya ya Rungwe na kwamba nyumba 18 za wananchi zimebomoka huku zingine zikiwa zimezingirwa na maji.

Alisema kaya 264 zimekosa makazi kwa muda, hatua iliyowalazimu kutenga maeneo matano yakiwemo maeneo ya shule, ofisi za vijiji na kwenye makanisa kwa ajili ya kuwahifadhi waliokosa makazi kuwahudumia mahitaji muhimu.

"Athari hizo zimesababisha kufungwa kwa muda kwa shule nne za msingi na sekondari, miundombinu ya barabara zote katika maeneo yetu imeharibika na kushindwa kupitika kabisa, lakini pia tunaendelea na tathimini ya mashamba yaliyoathirika," alisema Venusta.

Pia, alisema baadhi ya maeneo yaliyoathirika wameshindwa kuyafikia kutokana na kuharibika kwa miundombinu ya barabara zinazoelekea kwenye maeneo hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema Rais Samia alimkabidhi msaada kwa ajili ya wananchi hao wenye thamani ya Sh. milioni 35 na kwamba aliagizwa ipelekwe kwenye kaya zilizoathirika na mafuriko.

Alitaja vitu vilivyotolewa ni mikeka 300, magodoro 50, mablanketi 100, mashuka 50 pamoja na vyandarua 94 kwa ajili ya kujikinga na mbu, unga mifuko 50, maji ya kunywa katoni 100, sabuni katoni nne, ndoo 100 pamoja na sukari tani tatu.

Homera alimwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo kuanza uandikishaji wa majina ya wananchi ambao wako tayari kuhama maeneo hatarishi ndani ya mwezi mmoja ili watafutiwe maeneo mengine ambayo ni salama.

Mbunge wa Kyela, Ally Mlagila maarufu kwa jina la 'Kinanasi' alisema miaka yote wilaya hiyo imekuwa ikikumbwa na mafuriko ya mudu mfupi lakini msimu huu athari zimekuwa kubwa zaidi kutokana na mvua kunyesha mfululizo kwa zaidi ya wiki tatu.

Alisema pamoja na kukosa makazi upo uwezekano wananchi wake wakakabiliwa na njaa kutokana na mashamba kufunikwa na maji na hivyo akawaomba wataalamu kutoa elimu kwa wananchi kujiandaa namna ya kukabiliana na hali hiyo.



Mbunge wa Mbeya Mjini na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akizungumza na waathirika wa maporomoko ya tope katika kata ya Itezi, jijini Mbeya, alipowatembelea kwa ajili ya kuwafariji, juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Mitaa, vijiji inayotekeleza miradi yapokea mifuko 1,200 ya saruji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MBUNGE wa Njombe Mjini mkoani Njombe, Deo Mwanyika ametoa mifuko 1,200 ya saruji ya Sh. milioni 43 kwa vijiji na mitaa inakotekelezwa miradi ya maendeleo ya ujenzi kwa nguvu za wananchi

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi saruji hizo kwa viongozi wa vijiji na mitaa iliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Mwanyika alionya vitendo vya baadhi ya viongozi ambao walipewa saruji hapo awali na kuziuza ili kupata fedha.

Alisema kusitokee mtu akarudia kuuza ama kuhifadhi vibaya hadi kusababisha kuharibika na badala yake ziende moja kwa moja kukamilisha maboma yaliyoanzishwa na wananchi.

"Kama kuna mtu anajua hajaanza ujenzi hatutaarifu hapa hapa kwa sababu siku zote hii kitu inaitwa fedha na shetani anaitafuta kila wakati," alisema Mwanyika.

Mwanyika alisema mahitaji ya saruji kwa ajili ya kukamilisha maboma na vifaa vingine vya ujenzi ni makubwa lakini mifuko 1,200 kutoka kwenye mfuko wa jimbo na nyingine kutoka kwenye mshahara wake utasaidia kupunguza changamoto kwa miradi ambayo tayari imeanzishwa na wananchi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nundu, Innocent Mlange alisema katika vijiji na mitaa yao kuna miradi mingine imeanzishwa na wananchi na kisha kuishia njiani, hivyo saruji hizo zinakwenda kuwapunguzia mzigo wananchi kuchangia.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete alisisitiza viongozi wa mitaa na vijiji kwenda kuzilinda na kuzitunza saruji hizo ili zisiharibike na badala yake kwenda kufanya kazi iliyokusudiwa.

# CWT yaiangukia serikali kuwapandisha madaraja walimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimeiomba serikali kuongeza kasi ya kuwapandisha madaraja walimu kwa madai kuwa baadhi yao wamekaa kwenye daraja moja kwa muda mrefu hali ambayo inapunguza ufanisi wakazi.

Aidha, kimeiomba serikali kuharakisha upandishaji wa mishahara ya walimu kulingana na mabadiliko ya madaraja ili kuepuka manung'uniko miongoni mwa watumishi hao hasa wanaoelekea kustaafu.

Rais wa CWT, Leah Ulaya alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Maofisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri nchini (REDEOA) uliofanyika jijini Mbeya, ukilenga kujadili namna ya kutekeleza sera na mitaala mipya ya elimu ambayo utekelezaji wake unaanza mwaka huu.

Alisema licha ya serikali kuboresha maslahi ya walimu, yapo baadhi ya madai ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka ikiwa ni pamoja na kupandisha madaraja kila mwaka na kwa wakati ili kuepusha uwepo wa pengo kubwa la madaraja.

Aliiomba serikali kuongeza ajira za walimu ili kuwapunguzia mzigo waliopo na kuongeza ubora wa elimu, huku akidai kuwa takwimu zilizopo hazina uwiano mzuri kati ya idadi ya walimu na wanafunzi.

Pia aliomba serikali kuajiri walimu hao kwa kuzingatia umri wao tangu walipohitimu kwa maelezo kuwa wapo baadhi yao wamekaa muda mrefu mtaani na hivyo wamekata tamaa ya kuendelea na taaluma hiyo ambayo anaamini wengi ni wito wao.

Katika hatua nyingine Rais huyo aliwataka walimu nchini kufanya kazi kwa ufanisi na kuwaamini viongozi wao kuwa wapo kwa ajili ya kusimamia maslahi yao na kuacha migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza ndani ya chama hicho ambayo alisema wanashughulika nayo kwa kufuata taratibu.

Kaimu Katibu Mkuu wa CWT, Joseph Misalaba alisema chama hicho kinajukumu la kuhakikisha walimu wote wanapata uelewa juu ya sera na mitaala mipya akisisitiza kuwa imeanzishwa kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa mwalimu pamoja na mwanafunzi.

Alisema CWT watakuwa bega kwa bega na walimu kuhakikisha wanapata elimu ya kutosha ili kukabiliana na mabadiliko ya mitaala hiyo kwa kuishauri serikali kutafuta njia nzuri itakayowezesha walimu wote nchini kupata mafunzo kuhusu mitaala hiyo.



# Wakili asema sheria ya vileo ni batili

**Na Mwandishi Wetu**

WAKILI wa Mahakama Kuu Zanzibar, Hassan Kijogoo, amesema Sheria Na. 9 ya Vileo inayoweka masharti kampuni tatu kupewa vibali vya uingizaji wa vileo Zanzibar ni batili kwa sababu inakwenda kinyume cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Kijogoo aliyasema hayo kutokana na hukumu iliyotolewa na Jaji George Kazi wa Mahakama Kuu ya Zanzibar ambayo imeeleza kuwa kifungu cha 33 (1} cha sheria hiyo kinavunja Katiba ya Zanzibar na sheria ya ushindani na kumlinda mlaji namba tano ya mwaka 2018.

"Hicho kipengele walichokuwa wakikitumia kinachweka masharti mwisho kampuni tatu za uingizaji wa vileo Zanzibar hakipo kwa mujibu wa hukumu ya mahakama na sasa hakipo, hivyo kampuni zote zinaruhusiwa kuingiza vileo bila masharti," alisema.

Wakili Kijogoo alisema kama watu wametimiza masharti, hakuna sababu ya kuwazuia bali jambo muhimu wanatakiwa kulipia leseni ambayo gharama yake ni Sh. Milioni 30 na kwamba kuruhusu kampuni zaidi ya tatu kutaongeza mapato kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA} na ile ya Zanzibar (ZRA).

"Hizo kampuni ziko tayari kulipa Sh. milioni 30. Sasa kama kuna wawekezaji wamejitokeza kuwekeza na wako tayari kulipa ni mtaji kwa serikali ambayo kupitia bandari, TRA na ZRA inapata kodi na kuongezeka kwa mapato," alisema.

Kijogoo alisema kwa msingi huo, kifungu cha sheria kilichokuwa kikizuia zaidi ya kampuni tatu kuingiza vileo Zanzibar ni batili na sasa Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar haipaswi kukitekeleza tena kwa mujibu wa hukumu iliyotolewa na mahakama.

Alisema sheria hiyo ilikuwa inakwenda kinyume cha kifungu 12 (1) (20 cha Katiba ambacho kinasema hakuna sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taathira yake.

Wakili Kijogoo alisema kwa msingi huo, mamlaka za serikali zinapaswa kuruhusu makontena 25 yanayoendelea kushikiliwa katika bandari ya Malindi, Unguja, baada ya kudaiwa kuingiza vileo bila kuwa na leseni ya uingizaji wa vileo.

Alisema uamuzi huo wa mahakama umekuja baada ya kampuni ya QMB kufungua malalamiko dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar baada ya kuzuiwa kuingiza vileo Zanzibar pamoja na kampuni zingine zenye sifa na uzoefu wa zaidi ya miaka 30 katika biashara hiyo.

Sakata la vibali vya uingizaji wa vileo Zanzibar limesababisha uhaba mkubwa wa pombe baada ya kupewa kampuni tatu ambazo hazina sifa na uzoefu katika biashara hiyo na kunyimwa kampuni tatu zenye uzoefu zilizokuwa zikiingiza vileo Zanzibar ambazo ni SCOCH, ONE STOP CENTER na ZMMI.

## Mwegelo asisitiza viongozi ushirikiano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Jokate Mwegelo, amesisitiza ushirikiano kwa viongozi ili kuwaunganisha vijana na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Akizungumza juzi baada ya ziara ya kwanza kisiwani Unguja baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo hivi karibuni katika viwanja vya Gymkana, alisema umoja na mshikamano ni nyenzo muhimu ya kuendeleza chama na jumuiya zake.

Mwegelo alisema jukumu kubwa la vijana ni kuelezea mazuri yanayofanywa na viongozi wao ambao wanafanya kazi nzuri na kuvuka malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, jambo ambalo linazidisha imani kwa wananchi, hivyo kukipa ushindi chama katika uchaguzi wa mwaka 2025.

Pia aliwapongeza vijana wa Zanzibar kwa mapokezi mazuri yanayothibitisha kuwa UVCCM ni nguzo ya CCM sambamba na kuwataka kuitumia ofisi ya vijana kwa kujadili masula yanayowahusu na si kupeleka fitna na uchochezi.

Kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar alisema umeleta maendeleo, umoja na mshikamano na kuahidi kudumisha, kulinda na kuenzi kwa maslahi ya vijana na taifa kwa jumla.

Naibu Katibu Mkuu UVCCM Zanzibar, Abdi Mahmoud Abdi, aliahidi kushirikiana na viongozi mbalimbali katika ngazi ya matawi, wadi, majimbo na wilaya ili kuhakikisha vijana wote wanapata fursa mbalimbali zilizopo pamoja na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote yanayotolewa na viongozi wakuu wa kitaifa wa chama na serikali.

Pia aliwakumbusha vijana waliokabidhiwa nafasi mbalimbali za uongozi kuwashika mkono vijana wenzao ili kuleta maendeleo na kuwajenga kimaadili na kuwa viongozi bora wa baadaye.



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba mstaafu, Salum Juma Tindwa nyumbani kwake kwa Mchina, akiwa katika ziara ya kuwatembelea wazee mbalimbali wa chama hicho, Unguja jana. **PICHA: SIHAKA OMAR**

# Mwinyi ahimiza utafiti kupata njia udhibiti maradhi, majanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wataalamu wa maabara kuvifanyia utafiti vitu wanavyovichunguza yakiwamo maradhi ili kuyadhibiti kwa njia za kisayansi.

Akisoma hotuba ya Rais Mwinyi katika kilele cha Wiki ya Maabara Duniani Visiwani Zanzibar, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kufanya hivyo kutasaidia taasisi kudhibiti maradhi na kuzielekeza njia zinazoshauriwa kirahisi kutokana na kuwapo na ushahidi wa kisayansi.

Pia aliwataka wataalamu hao kuongeza nguvu kwenye taasisi za utafiti zikiwamo Taasisi ya Afya ya Binadamu (ZAHRI), Utafiti wa Mifugo (ZALIRI), Taasisi ya Utafiti wa Sayansi ya Baharini (ZAFIRI) ili kufikia malengo yaliokusudiwa.

Alisema maabara zote zina mchango mkubwa kwa maendeleo ikiwamo ya afya na huduma zinazotolewa kwa wananchi, hivyo serikali itaendelea kuimarisha maabara zote ili kuendeleza kazi za uchunguzi wa maradhi, vinasaba, kemikali na vyakula.

Akizungumzia Sera ya Maabara Zanzibar, alisema ni jambo zuri na utekelezaji wa kazi za vipimo hasa zinapokuwa zinatekelezwa na wadau tofauti ni vyema kuwapo na miongozo itakayosaidia kulinda mipaka ya kiutendaji, ubora na viwango vinavyojali maslahi mapana ya wanaotegemea huduma kwenye taasisi hizo.

Dk Mwinyi aliwasisitiza wataalamu hao kushirikiana na kufanya kazi na viongozi pamoja na mashirika ya kimataifa yanayoshughulikia maendeleo kwa lengo la kuleta maendeleo ya kweli kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Pia aliwataka wataalamu hao kufanya mapitio ya mipango kazi yao kila robo ya mwaka, miezi sita na mwaka ili kujifanyia tathmini ya mafanikio na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Tusisubiri mpaka Wiki ya Maadhimisho ya Maabara ndipo mkaanza kufanya kazi, kwa kufanya hivyo hatutaweza kufikia malengo. Serikali inakuamini na inakutegemeeni kupata mambo mazuri kutoka kwetu," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Amour Suleiman, alisema lengo la maadhimisho ya wataalamu wa maabara Zanzibar ni kuungana na wataalamu wengine Duniani na kuona umuhimu wa kazi za Kimaabara katika kutoa huduma kwa jamii.

Alisema dunia huadhimisha siku hiyo kwa wataalamu wa maabara za afya pekee, lakini kwa upande wa Zanzibar sekta tofauti zimeshiriki kuadhimisha wiki hiyo zikiwamo maabara za afya, kilimo, mifugo, maji (ZAWA) ili kuweka nadharia ya Afya mjumuisho.

Wakitoa salamu za wadau wa maendeleo, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Masuala ya Afya (ICAP) Tanzania, Haruka Maruyama, na Wangeci Gatei wa Shirika la CDC Tanzania, walisema kupitia maabara zilizojengwa na kuwa na miumdombinu imara Zanzibar sasa inaweza kujiamini na kuwa na uhakika wa kukabiliana na tishio lolote la mlipuko na kulinda afya za Wazanzibari yanapotokezea.

Pia waliahidi kuendelea kufanya kazi na serikali kupitia Wizara ya Afya na kwamba wizara hiyo imeandaa mwongozo wa uwendeshaji wa ufuatiliaji wa maabara utakaoweza kuimarisha na kugundua mapema magonjwa.

Wataalamu wa maabara walisema mbali na mafanikio hayo yanayoonekana katika sekta hiyo, bado wataalamu wa maabara wa Zanzibar hawajaitumia ipasavyo fursa iliyotangazwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuingia ubia wa uendeshaji wa Maabara za hospitali zilizopo nchini.

Pia walisema kada hiyo inakabiliwa na ukosefu wa waatalamu wahandisi wa vifaa tiba wa kuzifanyia matengenezo ya tahadhari mashine hizo pale zinapoharibika na kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi, hivyo kusabaisha hasara na zinanunuliwa kwa gharama kubwa.

# Tume yafuta uchaguzi chama cha wafugaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME huru ya uchaguzi ya Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) imebatilisha na kufuta matokeo ya uchaguzi uliofanyika Aprili 8, mwaka huu, ngazi ya taifa, kanda za kusini na kati, wilaya za Songwe, Mbarali na Igunga kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uvunjifu wa katiba.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Charles Malangwa, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa maazimio ya kikao kilichofanyika Aprili 16, mwaka huu, kujadili na kutoa uamuzi juu ya malalamiko na rufaa mbalimbali za wanachama waliokuwa wagombea wa nafasi za wilaya kanda na kitaifa.

"Uchaguzi huu ulifanyika Aprili 8, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma chini ya kifungu cha 45, 46 na 48 cha kanuni za uchaguzi za chama. Tume imefikia uamuzi wa mwisho wa kubatilisha na kufuta matokeo yote ya kitaifa, kanda za kusini za kati, wilaya za Songwe, Mbarali na Igunga na uchaguzi tajwa utapangwa tarehe nyingine na mchakato kuanza upya," alisema Manlagwa.

Malangwa alisema uchaguzi wa taifa uligubikwa na uvunjifu wa Katiba ya Chama cha Wafugaji Tanzania ya mwaka 2013 Toleo la 2023 Sehemu ya Nne Ibara ya 2.0 ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 33,34 (2),35(1-6),36 (1-5), 43(1(ii) na 47 (9),(11) na (13) ya Kanuni za Uchaguzi za Chama.

"Aidha katika ukumbi wa mkutano mkuu wa uchaguzi na wakati uchaguzi ukiendelea, kulifanyika uteuzi wa mgombea wa nafasi ya Naibu Katibu Mkuu kinyume kabisa cha Kanuni ya 33 na 47 (13) ya Kanuni za Uchaguzi wa Chama," alisema.

Pia alisema kulifanyika kampeni za mabango na vipeperushi vya mgombea nafasi ya mwenyekiti Mrida Mshota Marocha na mgombea nafasi ya Katibu Mkuu, Mathayo Mgusa, ndani ya ukumbi wa mikutano wa uchaguzi kinyume cha Kanuni ya 34 (2) na 43 (1(ii).

"Pia kuteuliwa wasimamizi wengine kinyume cha katiba ya chama sehemu ya nne ibara ya 2.0 ikisomwa kwa pamoja na kufungu cha 35 (1) na (2) cha kanuni za uchaguzi za chama baada ya Ramadhani Ighandu, Mbunge wa Singida Kaskazini na Boniface Getare, Mbunge wa Bunda Vijijini, kujigeuza kuwa wasimamizi wa uchaguzi huo na kupora madaraka ya tume," alisema.

Aidha, alisema daftari la wapigakura halikuzingatiwa kinyume cha kanuni ya 36 (1-5), wajumbe waliohudhuria ukumbini na kupiga kura ni mara mbili zaidi ya wajumbe halali wa mkutano mkuu wa chama chini ya ibara ya 3.3 sehemu ya tano ya Katiba.

"Kwa mujibu wa kanuni ya 45 na 46 ya kanuni za uchaguzi za chama natangaza rasmi kuwa uchaguzi mkuu wa tarehe 08, Aprili 2024, haukuwa katika misingi ya huru na haki ili kutenda haki na ionekane imetendeka,tume inafuta na kubatilisha matokeo yote ya uchaguzi tajwa hapo juu, mchakato utaanza upya na ratiba itatangazwa huu ni uamuzi wa mwisho," alisisitiza Malangwa.



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali akizungumza na wakazi wa kijiji cha Mkiko, wilayani humo juzi, wakati akisikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Matumaini makubwa wananchi mradi uchimbaji

**Na Judith Julius,** NGARA

MKUU wa Wilaya ya Ngara, Mathias Julius, amesema wananchi wa Ngara mkoani Kagera wana matumaini makubwa ya mradi wa uchimbaji wa madini unaoendeshwa na kampuni ya Tembo Nickel.

Julius alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akiukaribisha ugeni wa maofisa kutoka kampuni hiyo katika ofisi yake, mjini hapa.

Ugeni huo uliongozwa na Meneja Mkuu wa Tembo Nickel, Rebecca Stephen, ambao pamoja na mambo mengine maofisa wa kampuni hiyo walikwenda katika ofisi hiyo kutambulisha wakandarasi washauri (IBIS).

Viongozi hao walipata wasaa wa kuzungumzia mambo mbalimbali yahusuyo mradi yanayoendelea kutekekezwa.

Julius alisema vijana wa kike na wa kiume katika wilaya ya Ngara watanufaika kwa kupata ajira katika mradi huo.

Viongozi wa kampuni ya Tembo Nickel pia walizungumzia malipo kwa wananchi wanaotakiwa kupisha mradi huo ambao kwa kiasi kikubwa wameshalipwa.

Meneja Mkuu wa Tembo Nickel, Rebecca Stephen, alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa mapokezi yake na kukubali kuwa mshauri wa mradi kwa kipindi chote kampuni hiyo itakapokuwa na uhitaji.

Alimshukuru pia Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kuipa kampuni hiyo ushirikiano ili kuona ndoto ya taifa ya kuanza kuwa mradi huo mkubwa wa kimkakati inatimia chini ya uongozi madhubuti na maelekezo yake.

Kwa mujibu wa Julius, serikali ya awamu ya sita inaendelea kuvutia wawekezaji ili kuendelea kukuza na kujenga uchumi imara kwa manufaa makubwa ya taifa.

## Hospitali zanufaika msaada vifaa tiba

**Na Maulid Mmbaga**

HOSPITALI sita za Jeshi la Polisi katika mikoa mbalimbali nchini zimepatiwa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 235.5 kutoka Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Usalama wa Raia (URA SACCOS) ili kuboresha huduma za afya kwa jamii.

Vifaa hivyo vinajumuisha mashine za 'X-Ray', Ultrasaund, ya kukanda mwili (massage machine), kupima figo na njia ya haja ndogo, kupimia seli, kuotesha wadudu wanaotumika kupima ubora wa dawa na vifaa vya kupimia watu wanaoenda kufanyiwa upasuaji.

Akizungumza jana Dar es Salaam baada ya kupokea vifaa hivyo, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, alisema msaada huo umefika wakati muafaka ambako jeshi la polisi liko katika hatua mbalimbali za maboresho.

IGP Wambura aliongeza kuwa hiyo itawaletea urahisi mkubwa pale watakapoamua kufanya ushirikishaji wa jamii katika kupambana na uhalifu.

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 571/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU EMANUEL RICHARD MASANCHE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JEROME MATTAO LUANDA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 09 mwezi 05 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 19 mwezi 04 mwaka 2024.

HAKIMU

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.19390 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE: SELINA MELKION HAULE-DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY**
**MARIA MELKION MBEYA--------PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and administration of Estate rules,CAP352 R E 2019)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 30 day of April /2024.
Dated at Morogoro this 28th day of March 2024.

Senior resident magistrate
Morogoro District Court

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BUSEGA**

**Kituo cha MKULA Mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 60 Mwaka 2024**

**Jina la Mdai PETER MWIKABE**

**Jina la Mdaiwa JOSEPH MISUNGWI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za Mashauri ya Madai Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa JOSEPH MISUNGWI**
**K.K**
**M/KITI WA KITONGOJI**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) UNADAIWA TSHS 600,000/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 23 Mwezi 04 Mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 Mwezi 04 Mwaka 2024

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MKULA

---

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6071 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late of the late FAUSTIN BENEDICT BONGOLE of Mlimwa C within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY THERESIA ABEL MOSHIRO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 07 Day of 05, 2024
Date at Dodoma this **19 Day of MARCH, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/C
DODOMA REGION

---

**KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI**

**VICTORY ROLAND NATAI** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 606 ANY** aina ya **TVS KING.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/47859/2024.**

# Matumizi yakijeshi yaongezeka duniani

**STOCKHOLM,** Sweden

TAASISI ya Kimataifa ya Utafiti wa Masuala ya Amani na Usalama (SIPRI), imesema matumizi ya kijeshi kote duniani yameongezeka kwa asilimia saba, ikiwa ni sawa na ongezeko la matumizi ya fedha ya dola trilioni 2.43 kwa mwaka 2023.

Taasisi hiyo ya SIPRI iliyoko mjini Stockholm, Sweden, ilisema ongezeko hilo la asilimia saba ni kubwa tangu mwaka 2009 huku ikiongeza kwamba nchi kumi zilizokuwa na matumizi makubwa ya kijeshi kwa mwaka 2023 zimeongozwa na Marekani, China na Russia.

Nan Tian, Mtafiti Mkuu katika mpango wa uangalizi wa matumizi ya kijeshi na utengenezaji wa silaha wa SIPRI, alisema ongezeko linaloonekana limetokana na kudorora kwa amani na usalama wa dunia.

Alisema mataifa yanaweka mbele nguvu za kijeshi na matokeo yake ni kuhatarisha usalama wa dunia, akitolea mfano mataifa ya Russia kwamba imeongeza matumizi yake kwa asilimia 24 ambayo ni sawa na dola bilioni 109. Ukraine imeongeza kwa asilimia 51, sawa na dola bilioni 65 na kupokea angalau dola bilioni 35 za msaada wa kijeshi kutoka kwa Mataifa ya Magharibi.

"Nchi wanachama wa Jumuiya ya kujihami ya NATO zimetumia takriban asilimia 55 ya matumizi ya kijeshi duniani," ilisema SIPRI.

Mtafiti mwengine wa SIPRI, Lorenzo Scarazzato, alisema miaka miwili ya vita vya Russia nchini Ukraine imebadilisha kabisa muonekano wa usalama na kutoa kitisho zaidi cha usalama badala ya amani na uthabiti duniani.

Katika Mataifa ya Afrika, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) iliongeza matumizi yake kwa asilimia 105, ikiwa moja ya nchi iliyo na matumizi makubwa mno ya kijeshi, mwaka 2023 na watafiti wanasema ongezeko hili bila shaka limetokana na mgogoro unaoendelea kati ya serikali, na makundi yaliojihami ya waasi. **DW**

# Wananchi Niger washinikiza vikosi vya Marekani kuondoka

**AGADEZ,** Niger

MAMIA ya watu wameandamana katika mji wa Agadez nchini Niger ili kupinga uwepo wa wanajeshi wa Marekani katika taifa hilo ambalo liko chini ya utawala wa kijeshi.

Hayo yanajiri wakati ujumbe kutoka Washington ukitarajiwa kuwasili nchini humo siku chache zijazo ili kupanga mikakati ya kujiondoa katika taifa hilo linalotawaliwa na jeshi.

Maandamano hayo yalishuhudiwa katika mji wa kaskazini mwa jangwa wa Agadez, kunakopatikana kituo cha anga cha Marekani na yaliitishwa na kundi la vyama 24 vya kiraia ambavyo vimekuwa vikiunga mkono serikali ya kijeshi tangu mapinduzi ya mwaka jana.

Baada ya hayo kujiri Marekani iliafiki kuwaondoa wanajeshi wake zaidi ya 1,000 katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi ambako Marekani ilijenga kambi yake kubwa ya kijeshi yenye thamani ya dola milioni 100 ambayo pia ilikuwa ikitumiwa kurusha droni zake.

**Jeshi la Niger lilitangaza kuvunja makubaliano ya ulinzi na Marekani, kwa madai kuwa yalifikiwa chini ya shinikizo na kwamba kuwepo kwa wanajeshi wa Marekani nchini humo ni kinyume cha sheria.**

Miongoni mwa mabango yaliyobebwa na waandamanaji hao yalisomeka "Hii ni Agadez, sio Washington, jeshi la Marekani nendeni nyumbani".

Issouf Emoud, ambaye anaongoza Vuguvugu la M62 katika mji huo, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba ujumbe wao uko wazi akieleza kuwa "Wanajeshi wa Marekani wapakie virago vyao na kurudi nyumbani".

Aidha, ilielezwa kuwa mwanaharakati huyo aliratibu pia maandamano ya kutaka kuondoka kwa vikosi vya Ufaransa ambavyo vilijiondoa rasmi mwaka jana. Ikielezwa kuwa kwa muda mrefu Niger imekuwa nchi ya mkakati kwa Marekani na Ufaransa katika azma yao ya kupambana na makundi ya kigaidi katika eneo la Afrika Magharibi.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mwezi uliopita, Jeshi la Niger lilitangaza kuvunja makubaliano ya ulinzi na Marekani, kwa madai kuwa yalifikiwa chini ya shinikizo na kwamba kuwepo kwa wanajeshi wa Marekani nchini humo ni kinyume cha sheria.

Kiongozi wa mashirika ya kiraia, Amobi Arandishu, alisema kutumwa kwa jeshi la Marekani nchini Niger hakuna manufaa kwa usalama wao, na kusisitiza kuwa makundi yenye silaha bado yanaendelea kuzusha vurugu katika maeneo ya jangwani, na kwamba mataifa ya Urusi, Marekani, Ujerumani, Ufaransa, wote wanakuja Niger kwa maslahi yao wenyewe.

Baada ya mapinduzi yaliyomuondoa madarakani rais wa Niger aliyechaguliwa kidemokrasia Mohamed Bazoum, utawala wa kijeshi ulivitimua pia vikosi vya wakoloni wao wa zamani Ufaransa mwishoni mwa mwaka 2023.

Vile vile, vyombo vya habari nchini humo, vilisema wakufunzi wa kijeshi wa Russia waliwasili Niger mwezi huu wakiwa na vifaa kadhaa vya kijeshi pamoja na mfumo wa ulinzi wa anga, hatua iliyofikiwa baada ya mazungumzo kati ya mtawala wa kijeshi Jenerali Abdourahamane Tiani na Rais wa Russia Vladimir Putin. **DW**




Wananchi wa Niger wakiandamana huku wakionyesha mabango yenye jumbe zinazoshinikiza wanajeshi wa Marekani kuondoka katika taifa hilo, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Miili 300 yabainika kwenye kaburi la pamoja Gaza

**GAZA,** Palestina

WAFANYAKAZI wa Ulinzi wa raia wamegundua kaburi la pamoja lenye takriban miili 300 na kulifukua katika hospitali ya Nasser kusini mwa Gaza na baada ya kuondoka kwa vikosi vya Israel katika eneo hilo Aprili 7, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Ulinzi wa Raia wa Khan Younis huko Gaza, waliipata miili hiyo ya mashahidi kutoka kwenye kaburi la umati katika uwanja wa hospitali ya Nasser Medical Complex tangu kuondoka kwa jeshi la Israel katika ukanda huo.

Ilielezwa kuwa mji wa Khan Younis umeachwa katika hali mbaya huku makazi ya wananchi yakibakia magofu baada ya mashambulizi ya miezi kadhaa ya Israel.

Mkurugenzi huyo wa ulinzi wa raia alietambulishwa kwa jina moja Suleiman alidai kuwa baadhi ya miili hiyo ilipatikana ikiwa imefungwa mikono na miguu.

"Kulikuwa na dalili za kunyongwa shambani, hatujui kama walizikwa wakiwa hai au waliuawa. Miili mingi imeharibika," alisema.

Mwanaume mmoja katika eneo la tukio aliambia CNN kwamba bado hajapata mwili wa mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka 21, ambaye aliuawa Januari mwaka huu.

"Bado sijampata, tulikuwa tumemzika kule. Lakini hatuwezi kumpata, na tulitaka kumfanyia kaburi la heshima," Alisema. **CNN**

# WADADA SIMBA, YANGA SC KURARUANA ALHAMISI HII

Na Saada Akida

BAADA ya kuvuna pointi sita ugenini katika michezo miwili iliyopita, Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema malengo yao ni kuhakikisha wanasaka alama tatu katika kila mchezo ikiwamo mechi ijayo ya Derby dhidi ya Yanga Princess.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania mzunguko wa pili ulianza Aprili 15, mwaka huu, ambapo Simba Queens ilishinda dhidi ya Ceasiaa Queens ya Iringa na kisha kuondoka na pointi tatu tena dhidi ya Baobab Queens katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Jumamosi iliyopita.

Alhamisi wiki hii, Simba Queens watakuwa ugenini katika mchezo wa 'Derby' dhidi ya Yanga Princess utakaochezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

**Akizungumza na Nipashe juzi, Mgosi alisema baada ya kufanikiwa kuvuna pointi sita ugenini, wamerejea nyumbani na kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita kwa ajili ya kujiandaa na michezo iliyopo mbele yao.**

Alisema kwa sasa mchezo muhimu uliopo mbele yao ni dhidi ya Yanga Princess ambapo licha ya misimu kadhaa wamekuwa wakivuna pointi mbele ya wapinzani wao hao, lakini mechi hii wataingia uwanjani kwa tahadhari kubwa kukabiliana nao kutokana na kila timu kujiimarisha.

"Ligi imekuwa ngumu hasa hiki kipindi cha mzunguko wa pili ukiangalia kila timu imejipanga kutafuta pointi nyumbani na ugenini, tumefanikiwa kushinda mechi mbili za ugenini, hii haina maana kwamba tupo bora kuliko wengine.

"Hatutakiwi kuridhika na matokeo tuliyoyapata katika mechi za nyuma bali kujipanga zaidi kwa mechi zetu zijazo ambazo ni muhimu kushinda ili kufikia malengo yetu kwa msimu huu, kutafuta nafasi ya kwenda kucheza michuano ya kimataifa," alisema Mgosi.

Aliongeza kuwa ili kupata nafasi ya kwenda kucheza michuano ya kimataifa ni lazima kufanya vizuri katika ligi ya nyumbani kwa kufanikiwa kutwaa ubingwa wa ligi hiyo ambao waliupoteza msimu uliopita.

Simba Queens wanaongoza msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 31, wakifuatiwa JKT Queens iliyopo nafasi ya pili na alama 25 wote wakicheza michezo 11, Yanga Princess nafasi ya tatu pointi 21 wakicheza mechi 10 wakiwa na mechi moja mkononi dhidi ya Baobab Queens.




Msajili wa Vyama vya Michezo kutoka Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Wakili Evordy Kyando, akimkabidhi hati ya usajili, Mratibu wa Taasisi ya Tanzania Veterans Sports Promotion, Suleiman Methew, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Ligi Kuu ya Maveterani Tanzania Bara sasa yaja

Na Saada Akida

TAASISI ya Tanzania Veterans Sports Promotion kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), wameanzisha Ligi Kuu ya Maveterani Tanzania Bara inayotarajiwa kuzinduliwa rasmi Mei 14, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe Makao Makuu ya TFF jana, Mratibu wa Taasisi hiyo, Suleiman Methew, alisema Taasisi hiyo imesajiliwa rasmi na kutambulika na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), na wanaenda kushirikana na TFF kwa ajili ya kuanzisha ligi hiyo.

Alisema lengo la kuanzisha ligi hiyo ni kuwapa nafasi baadhi ya wachezaji ambao wanastaafu soka wakiwa na umri wa miaka 35, kucheza ligi hiyo ambayo bado hawajaweka wazi lini inatarajiwa kuanza.

"Tutakutana na TFF kupanga ratiba ya ligi na lini itaanza rasmi, pia usajili utakaofanyika utakuwa chini ya shirikisho hilo kwa kutoa kibali kwa mwaka mmoja, mmoja. Pia mchezaji aliyewahi kucheza Tukuyu basi anaweza kusajiliwa na Simba au Yanga Veterans," alisema Methew.

Aliongeza kuwa wachezaji watakaosajiliwa ni kuanzia miaka 35 na kuendelea, kwa sababu kuna baadhi ya nyota wanastaafu soka mapema na hawana la kufanya hali hiyo watawapa nafasi ya kucheza katika ligi hiyo ya Veterans.

Methew alisema TFF watakuwa na mamlaka ya kwenda katika ngazi mbalimbali ikiwamo wilaya na mikoa na baadaye itakuja taifa kama ilivyo kwa ligi zingine.

Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa TFF, Boniface Wambura, alisema wanashirikiana na taasisi hiyo na kuwapa ushirikiano wa kutosha kwa kuhakikisha wanasimamia ligi hiyo itakayochezwa kwa mwogozo.

"Hatuna mengi ya kusema zaidi ya kuwapongeza kwa hatua hii, tutawapa ushirikiano mkubwa katika kubafanikisha malengo ya taasisi hii ya kuanzisha ligi hiyo ambayo inawapa nafasi wachezaji wazamani wenye nguvu za kucheza michezo hiyo," alisema Wambura.

Naye Msajili wa Vyama vya Michezo wa BMT, Wakili Evordy Kyando, amekiri kuwapo kwa taasisi hiyo kwa ajili ya kuendeleza mchango kwa wachezaji ambao wamemaliza kucheza.

"Ni kweli tumesajili taasisi hii ambayo mbali na kuanza na soka, lakini hapo baadaye watakuwa na michezo mingine hasa kwa wachezaji ambao wanastaafu kucheza na kujikita katika michezo ambayo itaanzishwa na taasisi hii ya Tanzania Veterans Sports Promotion. Jambo muhimu ni kuhakikisha wanatumisha mfuko wao wa kifedha kwa lengo la kuja kusaidia wachezaji wenzao ambao watapata maradhi," alisema Kyando.

## Singida FG yazitaka tatu za Dodoma Jiji

Na Shufaa Lyimo

KLABU ya Singida Fountain Gate, imesema haijakata tamaa ya kumaliza nafasi za juu kwenye Ligi Kuu Bara na katika hilo wanaendelea kujipanga kuhakikisha wanapata pointi tatu kwenye mchezo wao ujao dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Singida FG kwa sasa ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi hiyo inayojumuisha timu 16, ikiwa ni baada ya kushuka dimbani mara 24 na kushinda mechi sita, sare nane huku ikipoteza michezo 10, hivyo kujikusanyia pointi 26.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ngawina Ngawina, alisema licha ya kupata pointi moja katika mchezo uliopita dhidi ya Mashujaa FC kwa sasa wanaelekeza nguvu zao katika mchezo huo dhidi ya Dodoma Jiji FC.

"Sasa hivi tunaelekeza nguvu zetu kwenye mchezo wetu huo ambao naamini utakuwa na upinzani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na timu zote," alisema Ngawina.

Aliongeza kuwa anawapongeza wachezaji wake kutokana na juhudi waliyoionyesha kwenye mchezo wao uliopita, na kuwataka wapambane ili kunusuru timu hiyo isishuke daraja.

Alisema malengo yake ni kupata pointi tatu katika michezo yao iliyobaki na kuomba mashabiki wao wasikatishwe tamaa kutokana na matokeo waliyoyapata.

"Ninaomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono wasikatishwe tamaa na matokeo tuliyoyapata tutapambana kuhakikisha tunaendelea kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao," alisema Kocha huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DIAZ ATAKIWA BARCA

BARCELONA ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Liverpool mwenye umri wa miaka 27, raia wa Colombia, Luis Diaz, msimu huu wa majira ya joto. ***(Sport)***

### AZINGATIWA WOLVES

KLABU ya Wolves inawazingatia golikipa wa Arsenal, Aaron Ramsdale, 25, kipa wa Liverpool na Jamhuri ya Ireland, Caoimhin Kelleher, 23, na kipa wa Sunderland, Anthony Patterson, kama wanaoweza kuziba nafasi ya kipa wa Ureno, Jose Sa (31), anayeondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### CITY KUMUUZA GREALISH

KLABU ya Manchester City ipo tayari kusikiliza ofa kwa kiungo wa kati wa England, Jack Grealish, 28, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ARAUJO SOKONI BARCA

BARCELONA itasikiliza ofa kwa mlinzi wa Uruguay, Ronald Araujo, 25, msimu huu, huku Manchester United ikionesha nia. ***(Sport)***

### PALACE YAMSAKA ONYEDIKA

KLABU ya Crystal Palace inaweza kujiunga na harakati za kumsaka kiungo wa kati wa Club Bruges raia wa Nigeria, Raphael Onyedika, 23. ***(Sun)***

### MENDY AWINDWA ARSENAL

ARSENAL, Liverpool na Manchester United ni miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili beki wa Real Madrid na Ufaransa, Ferland Mendy, 28. ***(L'Equipe)***

### MAATSEN KUBAKIZWA

BORUSSIA Dortmund italazimika kulipa kiasi cha kuvunja rekodi ya klabu cha pauni milioni 35 iwapo inataka kubadilisha mkopo wao kwa mlinzi wa Chelsea, Ian Maatsen, 22, kuwa mkataba wa kudumu. ***(Mirror)***

### AIT-NOURI ANYATIWA

KLABU ya Manchester City inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal na Liverpool katika mbio za kuwania kumsajili beki wa kushoto wa Wolves na Algeria, Rayan Ait-Nouri. ***(Mirror)***

### OMORODION AWANIWA EPL

KLABU za Ligi Kuu England, EPL, zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Atletico Madrid, Samu Omorodion, 19, ambaye yuko kwa mkopo Alaves. ***(AS)***

### VLAHOVIC BEI JUU

ARSENAL italazimika kulipa euro milioni 60 ikitaka kumsajili Mserbia, Dusan Vlahovic, 24, kutoka Juventus msimu huu wa majira ya joto. ***(Tuttosport)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inapanga kumnunua mlinzi wa Juventus mwenye umri wa miaka 19, Dean Huijsen, kwa pauni milioni 25, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo AS. ***(Mirror)***

## DONDOO SOKA
## MAGAZET LAYA



# TEN HAG: NI MAFANIKIO UTD KUTINGA FAINALI FA

**●●● Kucheza fainali mara mbili mfululizo, nilikuwa na hisia mchanganyiko, kwani…**

**LONDON,** England

ERIK ten Hag amekiri Manchester United "iliondokana nayo" baada ya kupoteza uongozi wa mabao matatu dhidi ya Coventry kabla ya kuhitaji mikwaju ya penalti ili kushinda nusu fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Wembley Jumapili, jijini London.

**United walikuwa mbele kwa mabao 3-0 katikati ya kipindi cha pili kabla ya Coventry kurudisha yote matatu ndani ya dakika 20 za mwisho.**

Timu hiyo inayoshiriki Ligi ya Championship ilifikiri kwamba ilifunga bao lingine mwisho wa muda wa nyongeza kabla ya VAR kulikataa.

United ilifuzu kwa mikwaju ya penalti wakati Rasmus Højlund alipofunga ya mwisho. Na sasa itacheza fainali ya pili mfululizo ya FA dhidi ya majirani zao Manchester City mwishoni mwa Mei.

"Ni wazi nilikuwa na hisia mchanganyiko," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Lakini ni mafanikio kuwa mara mbili mfululizo kwenye fainali ya Kombe la FA ndani ya miaka miwili. Unapokuwa na udhibiti mkubwa, ukitawala mchezo, mabao 3-0, tunapaswa kushinda.

"Jinsi ambavyo hatukufanya vizuri, na kutoka dakika 70 hadi mwisho tulifanya makosa. Mara kadhaa tulishushana chini. Lakini mwisho tuliwaondoa."

Ten Hag aliulizwa ikiwa ilikuwa ni aibu kushinda mchezo huo kwa mikwaju ya penalti dhidi ya timu inayoshiriki ligi ya chini.

"Hapana, siwezi kuona hilo," alisema.

"Mwisho wa siku inahusu mafanikio, mimi naona makosa tunayofanya, lakini si jambo la aibu, ni mafanikio makubwa.

"Wachezaji wanaona kwamba kuna hisia tofauti. Tuliwaruhusu kurejea kwenye mchezo na si lazima kabisa."

Licha ya kufika fainali ya Kombe la FA na kujitengenezea nafasi ya kushinda taji la pili katika misimu mingi kama kocha wa United, mustakabali wa Ten Hag pale Old Trafford bado haujafahamika.

Mholanzi huyo, alipuuzia mbali pendekezo kwamba ingawa United ilishinda, nafasi yake imedhoofishwa na mchezo dhidi ya Coventry.

# BARCELONA WALALAMIKIA TEKNOLOJIA YA GOLI



**BARCELONA,** Hispania

GOLIKIPA wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen na kocha, Xavi Hernandez, walilaumu kukosekana kwa teknolojia ya mstari wa goli nchini Hispania baada ya kupoteza kwa mabao 3-2 Jumapili dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa El Clasico.

LaLiga ni miongoni mwa ligi chache za daraja la juu barani Ulaya ambazo hazijaweka teknolojia hiyo, ikimaanisha kuwa iliachwa kwa VAR pekee na kuamuru kwamba Andriy Lunin alizuia bao la Lamine Yamal katika kipindi cha kwanza pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Madrid walishinda mchezo huo wa kusisimua, huku bao la ushindi la dakika za lala salama la Jude Bellingham likiwasogeza kwa pointi 11 dhidi ya Barca kileleni mwa msimamo wa ligi zikiwa zimesalia mechi sita pekee.

"Siwezi kupata maneno ya kuelezea kile kilichotokea kwenye mstari wa goli," alisema Ter Stegen akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni aibu kwa soka, kuna fedha nyingi kwenye mchezo huu, lakini sio kwa kile ambacho ni muhimu.

"Sielewi jinsi ambavyo hakuwezi kuwa na fedha kutekeleza teknolojia ambayo ligi zingine zinazo."

Xavi aliunga mkono maoni ya Ter Stegen, akielezea kupoteza mbele ya Madrid - kikiwa kipigo cha tatu cha 'Blaugrana' hao kwenye El Clasico msimu huu.

"Ninakubali kabisa maoni ya Ter Stegen," alisema Xavi katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mchezo.

# Klopp adai alicheza kamari dhidi ya Fulham



**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema alicheza kamari katika mabadiliko sita kwa timu yake ya Liverpool dhidi ya Fulham ili kuwaokoa wachezaji wake kutokana na kuchoshwa katika jitihada zao za kuwania taji la Ligi Kuu England.

Wakiwa wamepoteza pointi tano katika mechi zao mbili za mwisho za ligi, wakitoka sare ya mabao 2-2 na Manchester United kabla ya kufungwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Crystal Palace, ushindi wa 3-1 wa Liverpool pale katika dimba la Craven Cottage uliwapeleka hadi nafasi ya pili, sawa na vinara Arsenal na pointi moja mbele ya Manchester City.

Ikipata ushindi dhidi ya Everton kwenye mechi ya 'dabi' ya Merseyside kesho Jumatano utaifanya Liverpool kuwa pointi nne mbele ya City kabla ya safari yao ya kwenda kucheza na Brighton saa 24 baadaye.

Lakini baada ya wachezaji wake kushindwa kupindua matokeo ya mchezo wa kwanza wa mabao 3-0 katika mchezo wa mkondo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Atalanta nchini Italia, Klopp alisema hakuwa na chaguo la kuwapumzisha wachezaji muhimu, akiwemo Mohamed Salah na Alexis Mac Allister dhidi ya Fulham.

"Nilifanya mabadiliko kwa asilimia 100 kwa uhakika kwamba tulipaswa kufanya," alisema Klopp katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Tunacheza Jumatano kwa hiyo ninahitaji kufanya mabadiliko kabla ya wachezaji kunipa ishara wazi kwamba wamemaliza.

"Kwa vijana ni ngumu. Lazima upitie hili. Lakini vijana hawa wote wana ubora wa hali ya juu."

# Silva adokeza mustakabali wake Chelsea

**LONDON,** England

MSAHABIKI wa Chelsea hivi karibuni watajua hatima ya Thiago Silva katika Uwanja wa Stamford Bridge, kwani Mbrazil huyo tayari ameshafanya uamuzi wake iwapo atasalia au ataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto.

Silva alijiunga na Chelsea kutoka PSG kwa uhamisho wa bila malipo mwaka 2020 na alikuwa kiungo muhimu wa kikosi kilichoshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021. Pia alishinda Kombe la Klabu Bingwa Dunia akiwa na Chelsea mwaka uliofuata.

Akichukuliwa kama mmoja wa walinzi bora wa kizazi chake, Mbrazil huyo anasherehekewa kwa nidhamu yake na sifa za uongozi.

Kutokana na kupoteza mbele ya Manchester City katika nusufainali ya Kombe la FA Jumamosi, Silva alionekana kuwa na hisia kali, na pengine alitambua kuwa ingeweza kuwa fursa yake ya mwisho kupata medali akiwa na Chelsea, kutokana na mkataba wake kuisha Juni.

Kabla ya mechi, mke wa Silva alishiriki picha zake na familia yake wakijiandaa kutazama kutoka kwenye viwanja vya Wembley kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Katika chapisho moja, akiwa ameshikilia skafu ya Chelsea yenye jina la Silva, aliandika: "Ni ngoma ya mwisho Wembley."

Alipoulizwa kuhusu kuondoka London Magharibi, Silva alijibu (kupitia The Standard): "Utajua siku chache zijazo. Ni afadhali nisitoe maoni yangu sasa, hasa baada ya kupoteza.

"Nimesikitishwa na matokeo, lakini mapema au baadaye, habari itatoka. Nina uamuzi akilini mwangu, lakini si wakati wa kuushiriki.

"Miaka yangu minne hapa ilikuwa mizuri sana, si kwamba sikujiamini, lakini kwa umri wangu na ukali wa ligi hii ... ni nadra kuona wachezaji katika kiwango cha juu wakiwa na miaka 39.

"Sipendi kujizungumzia, lakini unaweza kuona hili. Ninaona nina miaka kadhaa ndani yangu ya kuendelea kufurahia soka."



HABARI MICHEZO

## Chama, Aziz Ki wawindwa Azam FC

INATOKA UKURASA 24

baye naye mkataba wake unatamatika mwishoni mwa msimu huu na Clement Mzize ambaye majuma yaliyopita aliongeza mkataba wa miaka miwili.

Akizungumza na Nipashe jana, Dabo alisema amewafuatilia wachezaji hao na kujiridhisha wako vizuri na tayari majina amependekeza kwa uongozi wao kwenye mipango yao ya usajili kwa ajili ya kuboresha timu kuelekea msimu ujao wa mashindano.

"Si Mzize pekee ndio tunataka bali kuna Diarra na Aziz Ki pale Yanga, Simba tunahitaji wachezaji wawili Chama na Kibu. Ni wachezaji wazuri, mambo yakienda vizuri ninaimani tutapata huduma za nyota hao," alisema Dabo.

Tayari Azam ilishaweka wazi kuwa imeulizia uwezekano wa kuipata huduma ya Mzize, ikisema inataka kupata mshambuliaji asilia wa nafasi hiyo kutokana na kuwa katika mvutano wa kuvunja mkataba straika wao, Prince Dube.

Dube tayari ameondoka Azam FC akishinikiza kuvunja mkataba na klabu hiyo huku akiweka wazi hana mapenzi tena na timu hiyo anataka kwenda kujaribu bahati kwingineko.

Mshambuliaji huyo raia wa Zimbabwe, ambaye amekuwa akihusishwa na Yanga, alifikisha kesi yake ya kimkataba na Azam FC, kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), lakini waajiri wake hao walishinda.

Kuhusu suala la ubingwa msimu huu, Dabo amesema kulingana na muelekeo wa timu yake wako katika reli ya kuwania taji hilo kutokana na tofauti ya pointi nne kati ya aliyekuwa juu yao, Yanga.

Katika msimamo Azam FC inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi 54 ilizozikusanya kutokana na michezo 24 na Yanga wanaongoza ligi kwa pointi 58, kwa michezo 22 huku Simba ikishika nafasi ya tatu kwa alama 46 ilizozipata kutokana na mechi 21 ilizocheza hadi sasa msimu huu.

# SIMBA WAENDA KUJARIBU BAHATI MUUNGANO CUP

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kutupwa nje kwenye robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika na kisha kuondoshwa Kombe la FA (CRDB Confederation Cup), huku ikiendelea kuvurunda kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Klabu ya Simba leo inatarajia kuwasili Zanzibar tayari kwa ajili ya michuano ya Kombe la Muungano.

Michuano hiyo ambayo imeanzia moja kwa moja hatua ya nusu fainali, inaanza kesho kwa KVZ FC kuikaribisha Simba katika Uwanja wa New Amani Complex saa 2:15 usiku na kesho Jumatano itakuwa zamu ya Azam FC kuvaana na KMKM SC uwanjani hapo na muda huo huo, ikiwa ni fainali ya pili. Washindi wa mechi hizo watakutana fainali uwanjani hapo Aprili 27, mwaka huu.

**Ni miaka 20 sasa imepita tangu michuano hiyo isimame kufanyika, ambapo msimu huu imerudi kwa kuanza na timu nne.**

Akizungumza na gazeti hili jana Kocha Mkuu wa timu ya KVZ FC, Ali Mohmed Ameir, alisema mipango yao ni kufika fainali katika mashindano hayo licha ya kukabiliwa na mchezo mgumu dhidi ya Simba ambayo ina uwezo na uzoefu mkubwa katika mashindano ya ndani na nje.

Alisema kikosi chake kimefanya mazoezi na tayari kimeshapata mechi moja katika michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, mchezo ambao aliangalia mapungufu yaliyojitokeza na kuyafanyia kazi mazoezini.

"Mchezo huu ni mgumu kwetu na tunawajua wapinzani wetu 'level' yao katika soka, hivyo tutatumia mbimu ambayo itatufanya tupate ushindi," alisema.

Akizungumzia maandalizi ya michuano hiyo, Katibu Mkuu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai, alisema kila kitu kimekamilika kuelekea mashindano hayo.

Alisema wanaendelea kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa.

Hata hivyo, aliwaomba Wazanzibar na Watanzania kwa Ujumla wote kwenda uwanjani katika kuyapa hamasa mashindano hayo.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Gerezani jijini Dar es Salaam wakicheza mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gamondi: Ni ngumu kushinda tena tano

INATOKA UKURASA 24

kikosi chake kipo tayari kwenda kukutana na timu kubwa ambayo imetoka kufanya vema mechi iliyopita, hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa.

"Kila mchezo unakuja na mipango yake mechi ya kwanza tulifungwa 5-0, mechi hii ni nyingine na tumejipanga vizuri kutumia vizuri uwanja wetu wa nyumbani na hatupo vizuri katika msimamo wa ligi, hivyo inabidi tupambane," alisema Mketo.

JKT Tanzania haijashinda mechi yoyote ile ikicheza uwanja wake huo wa nyumbani, ikicheza nne na kupoteza moja, ikiaanza kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Simba, kabla ya kulazimishwa suluhu dhidi ya Namungo, ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC, na nyingine kama hiyo dhidi ya Prisons, huku ikishika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi, ikiwa na pointi 22.

# *Klabu ya Tallis yatoa siri ya ubingwa kuogelea*

**Na Shufaa Lyimo**

WAOGELEAJI wa Klabu ya Tallis wametoa siri ya mafanikio baada ya kuibuka mabingwa kwenye mashindano ya Klabu ya Taifa ya Kuogelea yaliyomalizika juzi, Jumapili kwenye Bwawa la Kuogelea la Shule ya Kimataifa Tanganyika (IST), iliyopo Masaki, Dar es Salaam.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti baada ya ushindi huo, walisema siri kubwa ya mafanikio hayo ni kufuata vema maelekezo waliyopewa na Kocha wao Mkuu, Alexander Mwaipasi, pamoja na kufanya juhudi mazoezini.

Crissa Dillip mmoja wa wachezaji wa klabu hiyo, alisema mashindano yalikuwa na ushindani mkubwa, lakini alipambana mpaka kufanikiwa kuipa ushindi klabu yake huku akiahidi kufika mbali zaidi kupitia mchezo huo.

Alisema anashukuru ameweza kuvunja rekodi kwa kuhakikisha anapunguza muda na kuwataka wazazi kuwaruhusu watoto wao wajifunze mchezo wa kuogelea.

Naye Raya Angemi, alisema siri ya ushindi huo ni kutokana na mazoezi waliyokuwa wanayafanya mara kwa mara kwani bila hivyo wasingefika walipo sasa.

"Ninashukuru kwa matokeo haya kwani tumefanya juhudi kubwa mpaka tumefanikiwa, malengo yangu ni kufanya vizuri zaidi katika mashindano ya kimataifa," alisema Angemi.

Meneja wa Klabu ya Tallis, Hadija Shebe: "Tulijipanga kuhakikisha tunapata ubingwa, hii ni mara sita mfululizo Japokuwa kulikuwa na upinzani tumeweza kutetea kombe letu."

Wakati huo huo Mkurugenzi wa Ufundi wa Chama cha Mchezo wa Kuogelea Tanzania (TSA), Amina Mfaume, alisema waogeleaji hao wameonyesha ushindani mkubwa, kwani wengi wao wamefanikiwa kupunguza muda wao.

Klabu ya Tallis imebeba ubingwa huo baada ya kukusanya pointi 385 ikifuatiwa na Klabu ya Dar Swimming yenye pointi 330.

# Michezo

Jumanne Aprili 23, 2024

Nipashe





## ‘Ni mafanikio Utd kutinga fainali FA’

UKURASA 21


NDOTO YA AZAM FC...




Aziz Ki

Kibu Denis

Diarra

# GAMONDI: NI NGUMU KUSHINDA TENA TANO

## ●●● Asema kilichobaki Ligi Kuu kwa Yanga sasa ni kutafuta pointi tatu na si...

**Adam Fungamwango na**

**Saada Akida**

BAADA ya kuwasambaratisha watani zao wa jadi Jumamosi iliyopita kwa mabao 2-1, Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, leo saa 10:00 jioni watashuka kwa mara ya kwanza kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam kuwavaa Maafande wa JKT Tanzania.

Yanga itakuwa na kazi mbili, moja ni kusaka pointi tatu ili kuukaribia Ubingwa wa Tanzania Bara, lakini pia kutaka kuendeleza ubabe ambao iliufanya mechi ya mzunguko wa kwanza, ikiishindilia mabao 5-0, mechi iliyochezwa Agosti 29, mwaka jana, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, na kuzima ngebe za msemaji wa klabu hiyo, Masau Bwire, ambaye ameahidi kuwa watalipiza kisasi.

**Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema haamini kama wanaweza tena kufunga idadi kubwa ya mabao kama ilivyokuwa mzunguko wa kwanza, kwa sababu anafahamu wapinzani wao watakuja kivingine.**

“Hakuna mechi rahisi, tunacheza kwa ajili ya kushinda na kutafuta pointi tatu, si kushinda mabao mengi, ikitokea nafasi ya kufunga zaidi tutafanya hivyo, mechi ya kwanza tulishinda mabao 5-0, nakumbuka kuwa tulicheza Azam Complex siyo huku tunakocheza, leo, tunatumia uwanja mwingine, hatufahamu kama utakuwa rafiki, kikubwa sisi tunahitaji pointi tatu tu,” alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema kikosi chake hakikuwa na maandalizi ya kutosha kwa mechi ya leo, tangu walipocheza dhidi ya Simba Jumamosi iliyopita, ila tu wachezaji wake wamefanya mazoezi ya kujiweka sawa.

Aliwataja wachezaji ambao watakosekana katika mechi ya leo ni Joyce Lomalisa ambaye aliumia katika mchezo wa dabi, na Pacome Zouzoua ambaye bado mpaka sasa hajaanza kucheza mechi yoyote tangu alipoumia, Machi 17, mwaka huu, katika mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo na Azam FC.

Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, George Mketo, alisema


INAENDELEA UKURASA 23


# Chama, Aziz Ki wawindwa Azam

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Azam FC, Youssouph Dabo (pichani), ametaja wachezaji watano kutoka Simba na Yanga, ambao amewapendekeza kwa uongozi wa timu hiyo ili kupata huduma zao kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Kutoka Simba, Dabo anahitaji huduma ya kiungo mnyumbulifu, Clatous Chama, ambaye mkataba wake upo ukingoni na Kibu Denis kwa ajili ya kutaka kuimarisha kikosi chake kwa msimu wa 2024/25.

Kwa upande wa Yanga wachezaji Dabo anaotaka kufanya nao kazi ni kipa Djigui Diarra, Stephane Aziz Ki am-




INAENDELEA UKURASA 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042